# KUCHUNGUZA DHIMA YA MTINDO KATIKA TAMTHILIYA ZA KIHISTORIA: UTAFITI LINGANISHI WATAMTHILIYA ZA MORANI NA KINJEKITILE

FADHILI ELIFURAHA FADHILI

TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI MASHARTI YA KUPATIA SHAHADA YA UZAMILI (MA. KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2014

## UTHIBITISHO WA MSIMAMIZI

Mimi, Prof. Dkt. Sheikh T.S.Y.M. Sengo, nathibitisha kwamba nimeisoma tasnifu hii iitwayo:*"**Kuchunguza Dhima ya Mtindo katika Tamthiliya za Kihistoria: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya za Morani na Kinjeketile,***na nimeridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuwasilishwa kwa ajili ya Utahini wa Shahada ya Uzamili ya Fasihi kwa Kiswahili (M.A. Kiswahili-Fasihi) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

é é é é é é é é é é é é é é é é

Prof. Dkt. Sheikh T.S.Y.M Sengo

(Msimamizi)

é é ..........................................é é é ..

Tarehe

## HAKIMILIKI

Tasnifu hii au sehemu yake yoyote hairuhusiwi kukaririwa, kuhifadhiwa,Kubadilishwa au kuhaulishwa kwa mbinu yoyote ile: kielektroniki, kimekanika, kunakilishwa, kurudufiwa, kupigwa picha, au kurekodiwa kwa utaratibu wowote ule katika hali yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wake au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa niaba yake.

# TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi **Fadhili Elifuraha Fadhili**, nathibitisha kwamba tasinifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya Shahada yoyote.

é é é é é é é é é é é é ....................

Saini

é é é é é é é é é é é é ............é é é é é

Tarehe

# TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa baba yangu mzazi Elifuraha Fadhili Mbwambo na mama yangu Monica Elifuraha Fadhili, mke wangu Joyce Fadhili na watoto wetu wapendwa Elifuraha Fadhili, Neema Fadhili na Debora Fadhili, pia bila ya kuwasahau wataalamu na wanafunzi wote wa fasihi ya Kiswahili.

## SHUKRANI

Katika mafanikio yoyote, upo mchango wa kimawazo, kifedha ama kiutendaji na kwa sababu mafanikio ya kazi hii sikuweza kujitegemea mwenyewe kwa kila kitu, inanipasa kutoa shukrani zangu za pekee kwa watu ama taasisi zilizonifanikisha katika malengo yangu.

Nikianza na shukrani za pekee kwa yeye anayetupatia pumzi ya uhai na kutupatia riziki kubwa kubwa na ndogo ndogo ambaye ni Mwenyezi Mungu kwani katika mafanikio haya si kwa nguvu zangu bali ni kwa neema yake.

Wapo watu ambao inanipasa kuwafanyia iliyo haki kwa kuwataja katika kufanikisha katika tasnifu hii; shukrani za pekee kwa mwalimu na Msimamizi wangu Prof. T.S.Y.M Sengo kwa juhudi zake alizonifanyia kwa kusimamia na kuisahihisha kazi hii hadi kufikia ubora huu, hakika anapaswa kuheshimiwa kwa mchango wake na anastahili kuigwa kwa mazuri haya. Naweza kumbuka maneno yake ya kutia moyo ambayo mara nyingi alikuwa akiyatumia, ótusichokeô neno hilo lilikuwa likinitia moyo sana kwani alikuwa ananiambia mara nyingi kuwa ukiwa na mimi hauwezi choka. Mengi yaliyo katika kazi hii ni sehemu tu ya matunda ya ujuzi wake mkubwa na ushauri wake wa kitaalamu.

Ninapenda pia kumshukuru Prof. Emmanuel Mbogo kwa kunifanikisha katika kukamilisha tasnifu hii, kwani amekuwa akinitia moyo na kutoa muda wake mwingi kunielekeza kwani mara nyingi nilitaka kufahamu undani wa kazi yake ya tamthiliya

ambayo nimeitumia katika kazi hii. Siwezi kumsahau Msanii wa kazi ya kifasihi inayoitwa *Kinjeketile* [E.Hussein] kwani alikubali kutoa mawazo yake yaliyokamilisha kazi hii akiwa kama mtafitiwa, naomba Mwenyezi Mungu ambariki sana.

# IKISIRI

Lengo la utafiti huu kama lilivyobainishwa katika sura ya kwanza ilikuwa ni kuchunguza dhima ya vipengele vya kimtindo katika tamthiliya za kihistoria kwa kulinganisha tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile* ili kubaini vipengele vinavyowafananisha na kuwatofautisha wasanii wa vitabu hivyo katika kuliwasilisha suala la kihistoria. Utafiti huu ulitumia mbinu tatu za ukusanyaji data ambazo ni; maktaba, usaili na dodoso. Sampuli iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya madhumuni maalumu na uteuzi rahisi. Aidha data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi maudhui na uchambuzi linganishi. Utafiti huu uliongozwa na *Nadharia ya Elimumitindo katika Uchambuzi wa Matini za Kifasihi*. Utafiti umegundua kuwa, tamthiliya hizi zinatofautiana katika mbinu za kisanii na ubunifu. Tamthiliya ya *Morani* imetumia mbinu na lugha ya kitamathali wakati tamthiliya ya *Kinjeketile* imetumia lugha ya kawaida, rahisi na ya wazi zaidi. Aidha utafiti huu umebaini kuwa, tamthiliya hizi zinatofutiana katika kuwasilisha suala la kihistoria kwa sababu wasanii wanawasilisha historia ya jamii ya Tanzania katika vipindi viwili tofauti. *Morani* anawasilisha historia katika kipindi cha baada ya uhuru na hivyo kujadili juu ya historia ya harakati za kupambana na ukoloni mamboleo wakati *Kinjeketile* inajadili kwa uhalisia juu ya harakati za jamii za kusini katika kupambana na ukoloni mkongwe, yaani, ukoloni katika utawala wa Mjerumani. Kwa upande mwingine, ilibainika kuwa tamthiliya hizi kwa vile zimeandikwa na wasanii wa jamii moja ambao wameshuhudia na kupata masimulizi ya historia ya jamii yao. Wasanii hawa wanafanana katika kuwasilisha maudhui ya kazi zao ambapo wote kwa pamoja wanajadili juu ya mambo mbalimbali yaliyopo katika jamii kama vile; rushwa, harakati za ukombozi, usaliti, unyonyaji na ukandamizaji.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO WA MSIMAMIZI** .... ii
**HAKIMILIKI** .... iii
**TAMKO LA MTAHINIWA** .... iv
**TABARUKU** .... v
**SHUKRANI** .... vi
**IKISIRI** .... viii
**ORODHA YA MAJEDWALI** .... xiii
**ORODHA YA VIAMBATISHO** .... xv
**SURA YA KWANZA** .... 1
**1.0 UTANGULIZI** .... 1
1.1 Utangulizi .... 1
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti .... 2
1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti .... 4
1.4 Malengo ya Utafiti .... 4
1.4.1 Lengo Kuu .... 5
1.4.2 Madhumuni ya Utafiti .... 5
1.5 Maswali ya Utafiti .... 5
1.6 Umuhimu wa Utafiti .... 5
1.7 Mipaka ya Utafiti .... 6
1.8 Uzingativu wa Masuala ya Kimaadili .... 6
1.9 Matatizo ya Utafiti .... 8
1.10 Muundo wa Tasnifu .... 8

1.11 Hitimisho ....................................................................................................9

**SURA YA PILI ....................................................................................................10**

**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA...........10**

2.1 Utangulizi ....................................................................................................10

2.2 Dhana ya Fasihi Linganishi ....................................................................................................10

2.4 Vipengele vya Lugha ....................................................................................................13

2.4.2 Tashibiha ....................................................................................................14

2.4.3 Tashihisi ....................................................................................................14

2.4.5 Sitiari ....................................................................................................15

2.5 Tafiti kuhusu Tamthiliya za Kiswahili ....................................................................................................16

2.6 Pengo la Maarifa ....................................................................................................18

2.7 Kiunzi cha Nadharia ....................................................................................................18

**SURA YA TATU ....................................................................................................23**

**3.0 MBINU ZA UTAFITI ....................................................................................................23**

3.1 Utangulizi ....................................................................................................23

3.2 Eneo la Utafiti ....................................................................................................23

3.3 Kundi Lengwa ....................................................................................................24

3.4 Sampuli na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli ....................................................................................................25

3.4.1 Mbinu ya Uteuzi Rahisi ....................................................................................................26

3.4.2 Uteuzi wa Madhumuni Maalumu ....................................................................................................26

3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ....................................................................................................28

3.5.1 Mbinu ya Dodoso ....................................................................................................29

3.5.3 Mbinu ya Usomaji wa Maktabani ....................................................................................................31

3.6 Zana za Utafiti ....................................................................................................31

3.6.3 Dodoso ....................................................................................................32

3.6.4 Kinasa Sauti ...............................................................................................32

3.7 Uchambuzi wa Data.......................................................................................33

**SURA YA NNE .................................................................................................36**

**4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA......................................36**

4.1 Utangulizi .......................................................................................................36

4.2 Vipengele vya Lugha katika Tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile*..................36

4.3 Mdafao wa Ujitokezaji wa Vipengele vya Lugha katika Tamthiliya Teule .....38

4.4 Uteuzi na Matumizi ya Tamathali za Usemi ..................................................39

4.5 Matumizi ya Tamathali za Semi katika *Kinjeketile* ........................................49

4.6 Tamathali za Semi...........................................................................................50

4.7 Dhima ya Vipengele vya Lugha katika *Morani* na *Kinjeketile* ........................56

4.7.2 Kulinganishi na Kulinganisha Uteuzi wa Vipengele vya Lugha na Suala la Kihistoria ..............................................................................................................59

4.7.3 Kutofautiana ..................................................................................................60

4.7.4 Kufanana.........................................................................................................65

4.8 Dhamira za *Morani* na *Kenjeketile* ...............................................................65

4.8.1 Matabaka .......................................................................................................66

4.8.2 Nafasi ya Mwanamke .....................................................................................66

4.8.3 Uongozi Mbaya ..............................................................................................67

4.8.4 Rushwa na Usaliti ..........................................................................................67

4.8.5 Mapinduzi na Harakati za Ukombozi ............................................................68

4.8.6 Unyonyaji na Ukandamizaji...........................................................................68

4.8.7 Hali Ngumu ya Uchumi.................................................................................68

4.8.8 Hitimisho ......................................................................................69

**SURA YA TANO ........................................................................................71**

**5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ...................................71**

5.1 Utangulizi ..........................................................................................71

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ..........................................................71

5.4 Mapendekezo .......................................................................................80

**MAREJELEO ............................................................................................81**

**VIAMBATISHO ..........................................................................................88**

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Namba 3.1: Idadi ya Washiriki wa Utafiti................................................ 28

Jedwali Namba 4.1: Vipengele vya Lugha katika *Morani*...................................... 37

Jedwali Namba 4.2:Vipengele vya Lugha katika Kinjeketile ................................. 37

Jedwali Namba 4.3:Mdafao wa Utokeaji wa Vipengele vya Lugha Katika *Morani*...................................................................... 38

Jedwali Namba 4.4:Mdafao wa Ujitokezaji wa Vipengele vya Lugha katika Kinjeketile ............................................................................ 39

Jedwali Namba 4.5:Tamathali za Usemi Katika Tamthiliya ya *Morani*.................. 40

Jedwali Namba 4.6:Mdafao wa Ujitokezaji wa Tamathali za Usemi katika Morani....................................................................... 40

Jedwali Namba 4.7:Mifano ya Sitiari katika *Morani*.............................................. 42

Jedwali Namba 4.8:Tashibiha katika *Morani*......................................................... 46

Jedwali Namba 4.9:Mifano ya Tashihisi katika *Morani*......................................... 48

Jedwali Namba 4.10:Matumizi ya Takriri katika *Morani*....................................... 49

Jedwali Namba 4.11:Mdafao wa Ujitokezaji wa Tamathali za Semi katika Kinjeketile ............................................................................ 50

Jedwali Namba 4.12:Matumizi ya Sitiari katika *Kinjeketile*.................................... 51

Jedwali Namba 4.13:Maana za Sitiari.................................................................... 53

Jedwali Namba 4.14:Matumizi ya Takriri katika *Kinjeketile*.................................. 54

Jedwali Namba 4.15:Tashibiha katika *Kinjeketile*.................................................. 55

Jedwali Namba 4.16:Mfano ya Tashihisi katika *Kinjeketile*.................................... 56

Jedwali Namba 4.17:Dhamira katika Sitiari (*Morani*) ........................................... 57

Jedwali Namba 4.18:Dhamira katika Sitiari *Kinjeketile* ........................................ 58

Jedwali Namba 4.19: Mbinu za Kimtindo Zinazotofautisha *Morani na Kenjeketile* ........................................................ 63

Jedwali Namba 4.20: Kufanana katika Uteuzi wa Tamathali za Usemi .................. 65

Jedwali Namba 4.21:Kufanana kwa Dhamira Zinazowasilishwa na Vipengele vya Lugha ............................................................................ 66

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatishi 1: Mwongozo wa Maswali ya Usaili kwa Ajili ya Wanafunzi wa Fasihi, Walimu wa Fasihi na Watu wa Karibu wa Watunzi...... 88

Kiambatishi 3:Mwongozo wa Maswali ya Usaili Kwa Ajili ya Watunzi wa Tamthilia ya Morani na *Kenjeketile*............................................... 90

Kiambatishi 4:Dodoso kwa Walimu wa Fasihi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam..... 91

Kiambatishi 5:Dodoso kwa Wanafunzi Wakozi ya Fasihi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania....................................................................... 93

# SURA YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii ni sura tangulizi ambayo inatoa usuli wa tatizo la utafiti huu. Katika kubainisha tatizo la usuli wa tatizo na tatizo lililofanyiwa utafiti, sura hii inahusu usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na hitimisho. Kabla ya kuanza tupate historia fupi ya watunzi wa tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile.*kitabu cha tamthiliya cha Morani kimetungwa na E.Mbogo (1971) na kutolewa chapa ya kwanza mwaka 1993 ambapo katika kazi yake anaakisi na kusawiri misukosuko ya kisiasa na kiuchumi nchini Tanzania katika miaka ya 1980. E.Mbogo ni Profesa wa Drama na Fasihi ya Kiswahili na amefundisha vyuo vikuu mbalimbali ambapo kwa sasa anafanya kazi katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

E. Hussein (1970) ni mwandishi wa kitabu cha tamthiliya ya Kinjeketile ambapo msanii huyu aliandika kazi hii ya kisanii kwa kutumia tukio la kweli la kihistoria lilitokea kwa watu wa kusini wakati waafrika walipokuwa wakipambana na Wajerumani. Mwandishi anaonesha namna gani maji yalivyotumiwa kama kinga dhidi ya mashambulizi ya risasi ambapo iliaminika maji hayo yanauwezo wa kuwakinga wasidhuriwe na risasi. Kinjeketile alitumia maji kama ishara ya umoja, kinga na upendo ambapo alikuwa akiyahimiza makabila kuungana kufanya mapambano na Mjerumani. Msanii E.Hussein amekuwa mwalimu na mhadhiri wa fasihi kwa miaka mingi na anafaa kuigwa kwa mchango wake katika fasihi ya Kiswahili.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Lugha ina vipengele mbalimbali vya kimtindo ambavyo hutumiwa na wasanii wa kazi za sanaa. Matumizi ya vipengele hivyo hutegemea maudhui, wakati na muktadha maalumu. Hivyo basi, ili kuelewa maana na ujumbe wa matini ni lazima tuchambue lugha kupitia vipengele vyake ambavyo ndivyo hubeba maana na ujumbe. Mtindo ni sifa ya kipekee aliyonayo msanii, ni upekee wa msanii katika uteuzi wa maneno, msamiati, lugha na muundo wa kazi ya sanaa. Kila mwandishi au msanii ana upekee wake wa mtindo katika ubunaji wa kazi za sanaa. Hivyo basi, tunapochunguza ama kuchambua ujumbe wa kazi za kifasihi hatuwezi kuepuka vipengele vya kimtindo vya kazi hizo. Kama anavyoeleza Leech (1969) kazi ya fasihi haiwezi kueleweka vizuri bila kuwa na maarifa ya lugha ambayo ndiyo njia ya kujieleza.  Kwa hiyo, ili kuielewa kazi ya fasihi ni lazima kuchunguza nduni za kiisimu za lugha fulani na jinsi msanii anavyozitumia kwa kuzihusianisha na malighafi za kiisimu ili kuelewa kile kinachowasilishwa.

Kwa vile vipengele vya lugha kimtindo hubeba ujumbe wa kazi za fasihi, utafiti huu basi unaona ipo haja ya kuchunguza vipengele vya kimtindo vilivyotumiwa katika tamthiliya kwa kutumia mifano ya tamthiliya mbili yaani; *Morani* na *Kinjeketile*. Lengo hasa ni kutaka kuchunguza jinsi wasanii wa tamthiliya hizo wanavyofanana, kutofautiana na kuhusiana katika uteuzi wa vipengele vya kimtindo ili kuwasilisha suala la kihistoria katika jamii.

Katika kazi ya fasihi, fani ina vipengele vya kimtindo ambavyo hutumiwa na wasanii kuwasilisha ujumbe wa kazi za sanaa. Hivyo basi, utafiti huu umejikita katika kipengele kimoja cha mtindo ambacho ni lugha. Lugha kama kipengele cha mtindo,

ni kipengele muhimu sana katika ujenzi wa kazi za sanaa. Imeelezwa na baadhi ya watafiti kuwa maana ya kazi ya fasihi hujikita katika vipengele vya lugha kama vile sitiari, tashibiha, tashihisi, kejeli, methali, misemo na nahau (Mutembei, 2002; Mosha, 2002; Wamitila, 2003; Jilala, 2008 & 2010; Senkoro, 2011). Hivyo basi, utafiti huu utachunguza kipengele cha lugha ili kubaini ni namna gani wasanii wa tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile* wanatumia vipengele vya lugha kuwasilisha suala la kihistoria.

Kwa maana hiyo basi, utafiti huu ni utafiti linganishi ambao umelenga kulinganisha dhima ya mtindo katika tamthiliya za kihistoria kwa kulinganisha tamthiliya ya *Morani* (1971) iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo na tamthiliya ya *Kinjekeitile* (1969) iliyoandikwa na Ebrahim Hussein. Lengo ni kutaka kuibua vipengele vya kimtindo ambavyo vimetumika katika kuwasilisha suala la kihistoria katika jamii na kuvilinganisha kutoka kwa msanii mmoja na msanii mwingine. Katika fasihi linganishi, mlinganishi anaweza kulinganisha kazi za vipindi tofauti vya kihistoria ama kazi za waandishi tofauti wanaozungumiza suala moja, hivyo basi, utafiti huu umejikita katika taaluma ya fasihi linganishi na unalinganisha kazi za waandishi wawili ambao wametumia sanaa kujadili na kuwasilisha masuala ya kihistoria katika jamii kwa nyakati tofauti. Kwa kufanya hivi tutaweza kuona ni namna gani wasanii hawa wanatofautiana ama kufanana katika kutumia vipengele vya lugha kuwasilisha historia ya jamii.

Utafiti huu umeangalia suala la uhistoria ambapo katika jamii yoyote ile lazima ipitie vipindi mbalimbali vyenye kutengeneza historia ya jamii husika, ni dhahiri kuwa kuna mchango mkubwa sana wa historia katika kazi za kifasihi kwani husaidia kizazi

kilichopo na kijacho kufahamu wapi jamii inatoka, mahali ilipo na mahali inapoelekea, ambapo yale yanayoonekana kutofaa hukemewa na kuwa mfano wa yale yasiyohitajika nay ale ambayo katika historia yanafaa huendelezwa ili kuijenga jamii. Katika kazi za kisanaa huwezesha kuona namna wasanii waliopita walivyosanii kazi hizo na kipi cha kuboresha na kipi kinabaki kama historia. Kulingana na hoja hizo utafiti huu uliona ni vyema kuchunguza vipengele vya kimtindo katika kudhihirisha suala la kihistoria.

## 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Waandishi wa kazi za fasihi wanaweza kuelezea suala moja katika jamii kwa kutumia mbinu mbalimbali za kimtindo. Ingawa wataalamu wanaeleza kuwa mtindo huweza kumtofautisha mwandishi mmoja na mwandishi mwingine bado kuna haja ya kujua kuwa waandishi wa tamthiliya za kihistoria wanatumia mbinu zipi za kimtindo katika kuwasilisha historia ya jamii? Uteuzi wa vipengele vya kimtindo wanavyovitumia unafanana ama kutofautiana?

Hivyo basi tatizo la utafiti ni kwamba tamthiliya nyingi za kihistoria hazijafanyiwa uchunguzi wa kina na kuweka bayana jinsi vipengele vya kimtindo vinavyoweza kumtofautisha msanii mmoja na mwingine katika kuwakilisha suala la kihistoria. Hii itasaidia kuona ni jinsi gani wasanii wa tamthiliya hizo wanafanana ama kutafautiana katika uteuzi wa vipengele vya kimtindo wanapowasilisha suala la kihistoria hususani kipengele cha lugha**.**

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahsusi kama ifuatavyo:

### 1.4.1 Lengo Kuu

Utafiti huu unachunguza dhima ya vipengele vya lugha katika tamthiliya za kihistoria kwa kulinganisha tamthiliya za *Morani* na *Kinjeketile* ili kubaini vipengele vinavyowafananisha na kuwatofautisha wasanii wa vitabu hivyo katika kuliwasilisha suala la kihistoria.

### 1.4.2 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu una madhumuni matatu:

(i) Kubainisha vipengele vya lugha katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile*

(ii) Kubainisha dhima ya vipengele vya lugha vilivyobainishwa hapo juu

(iii) Kulinganisha na kutofautisha uteuzi wa vipengele vya lugha katika kuwasilisha suala la Kihistoria.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unajibu maswali yafuatayo:

(i) Ni vipengele vipi vya lugha vinavyojitokeza katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile?*

(ii) Vipengele vya lugha vilivyobainishwa katika namba (i) hapo juu vina dhima gani?

(iii) Uteuzi wa vipengele vya lugha katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile* unafanana ama kutofautiana vipi katika kuwasilisha suala la Kihistoria?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Umuhimu wa utafiti huu umejikita katika nyanja kuu tatu; kwanza, matokeo ya utafiti huu yataongeza maarifa katika nadharia na mbinu za utunzi wa tamthiliya

husus ani tamthiliya za Kiswahili. Pili, utafiti huu utatoa mchango katika maarifa ya taaluma ya fasihi linganishi nadharia na mbinu. Hivyo basi, utafiti huu utaweza kutumiwa kama marejeo, hususani katika fasihi linganishi. Kwa maana hiyo, utawasaidia wanafunzi na watafiti wengine kupata marejeo kuhusu fasihi linganishi na tamthiliya ya Kiswahili kwa ujumla wake.

Tatu, utafiti huu pia utakuwa ni changamoto kwa watafiti wengine kufanya utafiti kuhusu tamthiliya za Kiswahili hususani tamthiliya za kihistoria na vilevile utatajirisha maktaba ya chuo.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza na kulinganisha vipengele vya kimtindo katika tamthiliya za kihistoria. Zipo tamthiliya nyingi za kihistoria, na kwa vile siyo rahisi kuzishughulikia tamthiliya zote, utafiti huu ulijikita katika kuchunguza na kulinganisha tamthiliya ya *Morani* ya Emmanuel Mbogo na *Kinjeketile* ya Ebrahim Hussein tu kwasababu ndivyo mtafiti alivyovilenga. Aidha, mtindo una vipengele vingi vinavyotumika katika kujenga kazi za fasihi, utafiti huu haukulenga kuchunguza vipengele vyote vya kimtindo bali ulijikita katika kuchunguza kwa kina kipengele kimoja tu cha kimtindo ambacho ni lugha katika tamathali za semi kwa undani.

## 1.8 Uzingativu wa Masuala ya Kimaadili

Kipengele hiki kinalenga kujadili masuala ya kimaadili yaliyohusika katika utafiti huu na namna mtafiti alivyoweza kuzingatia maadili ya utafiti kabla, wakati na baada ya kukusanya data. Kwa mfano Padgett (2002) anabainisha kwamba, masuala ya

kimaadili huibuka katika aina zote za utafiti, na utafiti usio wa kitakwimu ukiwemo. Masuala ya kimaadili ambayo yanapaswa kuzingatiwa katika utafiti ni pamoja na usiri, uwazi, utiifu, ushiriki wa hiari ama kujitolea kwa wahojiwa bila kulazimishwa, kuomba idhini na ruhusa ya kufanya utafiti katika maeneo ya utafiti, na uvumilivu.

Suala la kimaadili ambalo mtafiti alisisitiza, ni kuwaomba washiriki kushiriki kwa hiari na kujitolea katika kutoa data. Schutt (2006) anasema kuwa, kwa watafiti, ni jambo muhimu sana kuhakikisha kwamba washiriki wa utafiti wanashiriki kwa kujitolea. Hii ina maana kwamba mtafiti alihakikisha kuwa wahojiwa wanaoshiriki katika kutoa data, wanatoa data hizo kwa hiari na uamuzi wao binafsi bila kushinikizwa. Hivyo basi, katika mchakato wa kufanya usaili na kugawa hojaji mtafiti alielezea lengo la utafiti kwa washiriki na kuwaomba wajitolee kwa hiari na kushiriki kikamilifu katika usaili na kujibu maswali yaliyomo katika hojaji. Vile vile, wakati wa kutoa maelezo tangulizi ya mwongozo wa maswali ya usaili funge na hojaji mtafiti aliweka bayana malengo ya shughuli ya utafiti. Hali kadhalika, alisisitiza kwamba wahojiwa wanaombwa kujibu maswali ya hojaji na usaili kwa hiari. Aidha, mtafiti alitumia muda huo kujadiliana na wahojiwa juu ya lengo kuu la utafiti na matarajio yake ili kupata mawazo, maoni na mtazamo wao. Kwa kuambiwa na kuelewa malengo ya utafiti huu, wahojiwa waliweza kutoa mawazo, maoni na fikra zao juu ya kile wanachofahamu kuhusiana na utafiti huu kwa uhuru zaidi, hivyo, kwa kufanya hayo, ilisaidia zoezi zima la utafiti na kurahisisha shughuli ya ukusanyaji wa data.

Aidha mtafiti aliheshimu ridhaa ya washiriki kabla ya kutumia zana za utafiti, hivyo basi, mbali ya usaili na dodoso, mtafiti alitumia zana za ukusanyaji data kama vile;

kinasa sauti na kamera. Kabla ya kutumia zana hizo, mtafiti aliwaeleza wahojiwa sababu ya kutumia na kuwaomba ridhaa yao. Wahojiwa pia walielezwa wazi kuwa kila kitu kitakachorekodiwa pamoja na picha zote zitakuwa ni siri na zitatumika kwa usiri mkubwa kwa ajili ya malengo ya utafiti huu tu na si vinginevyo. Wahojiwa walikubali na kuwa tayari kurekodiwa.

## 1.9 Matatizo ya Utafiti

Katika utafiti huu, mtafiti alikutana na matatizo kadhaa ambayo yaliifanya kazi ya kiutafiti kuwa ngumu, ila alijitahidi kuyatafuta. Mojawapo ya tatizo kubwa ilikuwa upatikanaji wa vitabu vya tamthiliya vilivyotumiwa katika utafiti huu ambavyo ni *Morani* na *Kinjeketile*. Vitabu hivi ilikuwa vigumu kuvipata mana kama kitabu cha kinjeketile hata wanafunzi wa sekondari hawakisomi kama kitabu cha kiada na katika maktaba ni vigumu kukipata. Vitabu hivi ni vya miaka mingi iliyopita, ila mtafiti alitafuta katika maktaba kuu ya mkoa wa Dar es Salaam akapata nakala na kuinakilisha hivyo kupata nakala ambayo imetusaidia katika utafiti huu. Tatizo la pili alilokumbana nalo mtafiti ni umbali wa kijiografia kutoka mahali anapoishi katika Mkoa wa Arusha hadi Dar es salaam kwenda kutafuta data. Mtafiti alilitatua hili kwa kutumia mda wa likizo kukusanya data za kiutafiti ambazo zimekuwa na msaada mkubwa katika utafiti huu.

## 1.10 Muundo wa Tasnifu

Utafiti huu umegawanyika katika katika sura tano, sura ya kwanza inahusu utangulizi wa jumla wa utafiti, masuala yanayohusiana na tatizo lililofanyiwa uchunguzi katika utafiti huu, yamejadiliwa na kutolewa maelezo ya kina. Sura ya pili inahusu utalii wa kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia, ambapo sura ya tatu inahusu mbinu za

utafiti. Katika sura hii, tunaonesha mbinu za ukusanyaji data, mbinu za uteuzi wa sampuli na kujadili mkabala uliotumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu. Sura ya nne inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data na sura ya tano, ambayo ndiyo sura ya mwisho, inahusu muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo.

### 1.11 Hitimisho

Sura hii imejadili juu ya usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, masuala ya kimaadili na muundo wa tasnifu. Aidha katika sura hii ya kwanza tatizo la utafiti limebainishwa na kuelezwa wazi na kwa undani zaidi.

# SURA YA PILI

# 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inatalii mapitio ya maandiko tangulizi, katika sura hii maandiko na tafiti mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti zitajadiliwa kwa kina na hatimaye kuibua pengo la maarifa ambalo liliweka msukumo kufanya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu sita ambapo sehemu ya kwanza inahusu dhana ya fasihi linganishi, sehemu ya pili inajadili juu ya mtindo, sehemu ya tatu ni lugha na vipengele vyake, sehemu ya nne ni tafiti kuhusu tamthiliya za Kiswahili na sehemu ya tano ni pengo la kimaarifa na sehemu ya sita kiunzi cha nadharia.

## 2.2 Dhana ya Fasihi Linganishi

Guyard (1964) anasema kuwa fasihi linganishi ni tawi la historia ya fasihi ambapo anadai ni somo la mahusiano, mapatano, na maelewano ya kimataifa baina ya kazi na maisha ya waandishi wanaotoka katika fasihi tofauti.

Wellek (1988) anaifasili fasihi linganishi kuwa ni somo linalojishughulisha na uhusiano wa vitu viwili ambapo vinaweza kuwa kazi ya mtu binafsi, waandishi au kundi la waandishi na binadamu au fasihi kwa ujumla. Kwa upande wake, Wellek (1988) anaiona fasihi linganishi kuwa ni somo la fasihi nje ya mipaka ya nchi moja, ni kujifunza uhusiano baina ya fasihi kwa upande mmoja na eneo lingine la maarifa mfano sanaa, falsafa, historia ya sanaa za jamii, sayansi, dini na mambo mbalimbali ya kijamii.

Wellek na Warren (1996) wanaielezea fasihi linganishi kuwa ni mbinu itumiwayo na wahakiki wengi wa fasihi hata wanasayansi kujadili njia maalum ya usomaji wa sanaa mbalimbali ulimwenguni. Wanakubaliana kuwa ni taaluma inayoshughulikia tofauti au kufanana kwa fasihi ya makundi mawili au zaidi ya kiisimu, kiutamaduni, kihistoria, kiitikadi, kiuchumi, kijamii na kimataifa, japokuwa fasihi linganishi inatumika kulinganisha kazi za fasihi za lugha tofauti.

Mfano, Kijerumani, kichina, Kiingereza, Kiswahili na nyinginezo, lakini bado inajishughulisha na fasihi ya lugha moja ikiwa kazi hizo asili yake ni nchi tofauti au utamaduni na vipindi tofauti ndani ya lugha hiyo. Mfano, tunaweza kulinganisha kazi za fasihi za Penina Mhando na kazi za fasihi za S.Azizi zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

Fasihi linganishi katika utafiti huu utatusaidia kuweza kuweka mipaka ya kiulinganishi na pia kujua taaluma ya fasihi linganishi ambayo ndiyo hasa utafiti huu umekusudia kufanya. Pia fasihi linganishi itatusaidia kujua ni namna gani tunaweza kufanya ulinganishaji wa kazi za fasihi na vipengele vipi vya kuzingatia katika ulinganishaji wa kazi za fasihi katika jamii yetu.

## 2.3 Mtindo

Wamitila (2008) anaelezea kuwa mtindo ni elementi muhimu sana katika kazi ya kifasihi, ili kuweza kubainisha sifa za kimtindo za kazi ya fasihi, mchanganuzi wa matini au kazi ya kifasihi anapaswa kuchunguza mambo mengi katika kazi inayohusika kama vile uteuzi wa msamiati wa mtunzi, miundo na mipangilio ya sentensi, uteuzi na matumizi ya tamathali za semi na jazanda, usawiri wa wahusika,

motifu na dhamira zinazokaririwa katika kazi za watunzi, usimulizi na mbinu za usimulizi wenyewe, na hata sifa za uakifishi hasa zinazoelekea kukiuka njia za kawaida za kuakifisha.

Kila mtunzi ana mtindo wake ambao ni tofauti na mtindo wa mtunzi mwingine katika uteuzi na utumizi wa vipengele vyote vya kimtindo. Hata pale ambapo watunzi na au waandishi wamekulia katika mazingira sawa, muktadha wa uandishi ni mmoja, jambo linaloandikiwa ni lilelile na kipindi cha kihistoria kinachoumba kazi za fasihi ni kimoja; watunzi hao lazima watatofautiana katika namna ya kutumia vipengele vya mtindo katika kazi zao. Uteuzi wa vipengele vya kimtindo hutegemea ubunifu wa kisanii alionao msanii, hivyo basi, mtindo hujumuisha vipengele vifuatavyo ambavyo vinahusiana sana kwani ni vinajumuishwa katika kipengele cha lugha:

(i) Uteuzi wa msamiati

(ii) Miundo na mpangilio wa sentensi

(iii) Uteuzi wa tamathali za semi

(iv) Usawiri wa wahusika

(v) Motifu

(vi) Lugha

(vii) Usimulizi

Vipengele hivi vya mtindo ndivyo vitakavyotumika katika uchambuzi na ubainishaji wa vipengele vya mtindo katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjekeitile* ili kuweza kufikia malengo ya utafiti huu. Kutokana na wingi wa vipengele vilivyobainishwa hapo juu, si rahisi kushughulikia vipengele vyote vya mtindo, hivyo utafiti huu

ulijikita katika kuchunguza baadhi ya vipengele vya lugha tu katika mtindo. Kwa kufanya hivi, utafiti huu ulichunguza vipengele vya lugha na jinsi vinavyotumika katika kuwasilisha suala la kihistoria, sehemu inayofuata inajadili kuhusu vipengele vya lugha.

## 2.4 Vipengele vya Lugha

Lugha ina vipengele mbalimbali ambavyo hutumiwa katika kazi za fasihi ili kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Vipengele vya lugha ni pamoja na tamathali za usemi, lugha ya mkato na jazanda. Ufafanuzi wa vipengele hivyo ni kama ifuatavyo:

### 2.4.1 Tamathali za Usemi

Tamathali za usemi ni vifananishi au viwakilishi vya dhana moja kwa dhana nyingine tofauti au zinazofanana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza, au kuubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu ya kishairi iliyokusudiwa na mtunzi. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), tamathali ya (za) usemi, hutumiwa kuelezea fungu la maneno, au hata neno, ambalo, limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine.

Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa, tamathali za usemi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana moja kwa kutumia dhana nyingine tofauti au zinazofana nazo ambazo hutumiwa kwa lengo la kupanua, kupuuza, kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida ili kuwasilisha ujumbe na maana iliyokusudiwa kwa hadhira. Senkoro (2012) anaainisha tamathali za usemi, kuwa ni sitiari, tashibiha, metonomia, tashihisi, majazi, taashira na kejeli. Mulokozi na Kahigi (1979) wanaeleza kuwa,

tamathali zinazotumika zaidi katika ushairi ni tashibiha, tashihisi, kejeli, metonimia na sitiari. Katika sehemu hii tutaelezea tamathali chache zitakazo tumika katika utafiti huu kulingana na malengo ya utafiti huu.

### 2.4.2 Tashibiha

Hii ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia waziwazi, kwa hakika, tashibiha ni usemi wa kimlinganisho utumiao maneno-viungio kama vile *mithili ya*, *kama kwamba*, *kama*, *kama vile*, *tamthili ya*, *sawa* nakadhalika, mifano kama; mweusi kama mkaa, mweupe mithili ya theluji na mrefu kama twiga. Mifano hii ni tashibiha kwa sababu inalinganisha vitu kwa kutumia viunganishi.

### 2.4.3 Tashihisi

Ni usemi ambao sifa ya uhai huhamishiwa kwenye kitu kisicho na uhai, aghalabu, tashihisi ni tamathali za usemi ambapo vitu visivyo na sifa walizonazo watu hupewa sifa hizo. Wamitila (2003) anaeleza kwamba tashihisi ni tamathali ya usemi ambapo vitu visivyokuwa hai au na uhai huwasilishwa au husawiriwa kwa namna sawa na binadamu ya kuweza kufikiri na kuhisi sawa na afanyavyo binadamu. Tashihisi hutumiwa zaidi na washairi ambao kwa mfano hawasiti kusema óókimya hakishi kunena, kitakapo kusimamia, fedha huita wazuri wakaitika labeka, maji baridi yaliubusu mwili wake mwororoôô. Katika mifano hii, kimya kimepewa sifa ya kibinadamu ya kuenea na kusimamia, fedha imepewa sifa ya kuita na maji yamepewa sifa ya kubusu. Hivyo neno kimya, fedha na maji vimetumika kama tashititi kwa kupewa uhai, yaani sifa za vitu vyenye uhai zimehamishiwa kwenye maneno hayo.

### 2.4.4 Takriri

Ni tamathali ya usemi ambayo hurudiarudia sehemu ya neno, neno ama sentensi kwa kusudio la kuonesha msisitizo katika kile kinachomaanishwa na mzungumzaji ama mwandishi. Hussein (1970) anaonekana akitumia takriri kwa kiasi kikubwa katika kitabu cha tamthiliya ya *Kinjeketile* kusisitiza mambo kadhaa kwa mfano óómaji, maji, majiôô ambapo takriri hii ililenga kuzungumzia suala la maji kama dawa ya kimuujiza katika kuwakinga dhidi ya risasi ambapo matumizi ya neno hilo kujirudia mara kadhaa humaanisha si maji ya kawaida.

### 2.4.5 Sitiari

Kahigi (1994) anafasili sitiari kuwa ni uhamishaji wa maana kutoka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine. Vikoa vya maana vinavyohusika katika uhamishaji huu huwa vinatofautiana angalau kwa sifa ya kisemantiki moja ya msingi. Kinachohamishwa ni tabia, umbo au kazi ya kitu kwa kuihusisha na tabia au umbo au kazi ya kitu kingine (Lakoff & Johnson, 1980) katika kazi ya Kahigi (1994). Ili kuielewa dhana ya sitiari, tutumie mfano huu: *Juma ni simba*.

Katika mfano huu, hatumaanishi kuwa *Juma* amegeuka kuwa *simba* yaani mnyama bali sifa za *simba* zinahamishiwa kwake, yaani, *simba* ana sifa ya ukali, kwa hiyo, ukali unaonasibishwa na simba unahusishwa na ukali wa *Juma*. Muundo wa sitiari una vipengele vitatu: kizungumzwa, kifananisho na kiungo (Lakoff & Johnson, 1980; Kahigi 1994). Kizungumzwa ni kitajwa, ambapo katika mfano wetu, ni *Juma*; kifananishi ni kitu kinachohusishwa na kizungumzwa na katika mfano wetu ni *Simba*, na kiungo ni tabia au sifa zinazounganisha kizungumzwa na kifananishi hapa ni ukali.

Hivyo basi kwa kuzingatia tamathali za semi zilizobainishwa na Senkoro (2012), utafiti ulichunguza vipengele vya lugha ambavyo vimejikita katika uhamishaji wa maana kutoka katika dhana moja kwenda katika dhana nyingine ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira.

## 2.5 Tafiti kuhusu Tamthiliya za Kiswahili

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu tamthiliya za Kiswahili lakini nyingi ya tafiti hizo zimejikita katika kuchambua vipengele vya lugha na maudhui kwa ujumla katika tamthiliya na si katika kuchunguza dhima ya mtindo katika tamthiliya zilizotumika katika utafiti wetu. Kazi hizo ni pamoja na ya Kingȏei (1987), Ligembe (1995), Ramadhani (2005) na Saleem (2013).

Kingȏei (1987) alifanya utafiti juu ya tamthiliya za Ebrahim Hussein. Katika uchambuzi wake, Kingȏei anaeleza kuwa tamthiliya za mtunzi huyu kama vile *Alikiona* (1970), *Wakati Ukuta* (1970) na *Arusi* (1980) zinazomchora msanii huyu jinsi alivyokua na kustawi kisanaa. Msanii huyu amebobea vilivyo katika matumizi ya vipengele vya fani kama vile lugha na maudhui.

Katika utafiti wake, Kingȏei (1987) alibaini pia kuwa Ebrahim Hussein ana uwezo na anamudu ipasavyo kutumia lugha kama mbinu au chombo cha kusafirishia ujumbe wake katika tamthiliya zake. Kama tulivyoona katika hoja za Nadharia ya Elimumitindo katika Uchambuzi wa Matini (*Theory of Stylistics*),lugha ni mbeleko ya kazi za fasihi kiasi kwamba athari ya kazi ya fasihi kwa hadhira kwa kiasi kikubwa inategemea sana aina ya lugha iliyoibeba kazi hiyo.

Pamoja na utafiti huo, tunaona kuwa utafiti wetu utatofautiana na utafiti wa Kingʼei kwa sababu utafiti wetu ni linganishi ambao utalinganisha kazi mbili za fasihi za watunzi tofauti ambao wameandika kuhusu masuala ya kihistoria ili kuona ni jinsi gani wanatofautiana ama kufanana katika vipengele vya kimtindo.

Ligembe (1995) amechambua matumizi ya sitiari katika kazi ya tamthiliya ya *Lina ubani* iliyoandikwa na Penina Muhando. Katika uchunguzi wake amejadili muundo na umbo la tamthiliya ya Kiswahili. Tofauti na watafiti wengine Ligembe amejikita zaidi katika umbo la tamthiliya ya Kiswahili na kubainisha aina za sitiari. Utafiti wake haukuonesha uhusiano uliopo baina ya aina ya sitiari na ujenzi wa maana katika tamthiliya. Tofauti na utafiti wa Ligembe, utafiti huu, ni utafiti linganishi ambao utalenga kulinganisha na kulinganua kazi za tamthiliya za waandishi wawili ili kubaini vipengele vya kimtindo vinavyowafananisha na kuwatofautisha katika kulijadili na kuwasilisha suala la kihistoria kwa hadhira yake.

Ramadhani (2005) alifanya utafiti wa matumizi ya sitiari katika tamthiliya ya *Morani* ya Emmanuel Mbogo na *Mashetani* yaEbrahim Hussein. Huu ni utafiti linganishi unaotumia nadharia ya elimumitindo ambapo umelinganisha tamthiliya mbili. Aidha katika ulinganishi hakuwa mbali na hitimisho la Mosha (2002) kuwa sitiari sahili ndiyo yenye mdafao mkubwa kuliko sitiari zingine katika tamthiliya zote.

Aidha alihitimisha kuwa sitiari hutumika katika ujenzi wa dhamira mbalimbali katika tamthiliya zote mbili. Tofauti na utafiti uliofanywa na Ramadhani, utafiti huu, unatoafautiana na utafiti wa Ramadhani kwa sababu utafiti huu hautajikita katika kipengele kimoja cha tamathali za semi bali utajikita katika kuchunguza baadhi ya

vipengele vya kimtindo ili kuona ni jinsi gani vipengele hivyo vinawafananisha na kuwatofautisha wasanii hao.

Saleem (2013) alifanya utafiti linganishi wa tamthiliya za *Mashetani* na *Kivuli kinaishi* katika tasnifu yake ya uzamivu alibaini kuwa tamthiliya za *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi* zinafanana na kuhusiana katika mbinu za kimtindo na maudhui yake. Tofauti na utafiti wa Saleem, utafiti huu utajikita katika kulinganisha vipengele vya kimtindo wakati Saleem yeye alijikita katika kulinganisha fani na maudhui. Vile vile utafiti huu utajikita katika kulinganisha tamthiliya za kihistoria tofauti na Saleem (2013) ambaye kiunzi chake cha ulinganishi kilikuwa suala la kijiografia baina ya watunzi wa tamthiliya teule.

## 2.6 Pengo la Maarifa

Pamoja na kuwa kuna tafiti ambazo zimefanywa kuhusu ulinganishaji wa kazi za tamthiliya, lakini ulinganishaji huo haukuzingatia masula ya kihistoria. Vile vile tafiti nyingi zimejikita katika kulinganisha fani na maudhui ya kazi za faishi, hivyo, bado inaonesha kuwa utafiti wa kina unahitajika ili kutafiti kwa kina jinsi vipengele vya kimtindo vinavyoweza kumtofautisha msanii mmoja na msanii mwingine, pengo hili ndilo ambalo utafiti huu umekusudia kuliziba. Ili kufikia lengo hilo, utafiti huu basi, utajaribu kuziba pengo hilo kwa kuchunguza dhima za Kimtindo katika tamthiliya za kihistoria kwa kutumia mifano ya *Morani* na *Kinjekitile.*

## 2.7 Kiunzi cha Nadharia

Katika utafiti na uchunguzi wa kazi za fasihi, zipo nadharia mbalimbali ambazo zinaweza kutumika kuchunguza na kuchambua kazi za fasihi. Aidha, ni dhahiri

kuwa, kila nadharia inaweza kufaa ama kutofaa kuzichambua kazi za fasihi kwa kuzingatia lengo la utafiti. Katika utafiti huu tungeweza kutumia nadharia za fasihi kama vile nadharia ya *Umuundoleo,* Ufeministi, umaksi na *Uumbuji* hizi zikiwa ni baadhi tu ya nadharia. Hata hivyo, nadharia hizi zilionekana kutofaa katika kuchunguza na kuchambua data za utafiti huu kutokana na malengo ya utafiti huu.

Hivyo basi, kulingana na malengo ya utafiti huu, nadharia ya elimumitindo imeonekana kuwa inaweza kufaa na kutuongoza katika kuchunguza na kuchambua data za utafiti huu. Nadharia ya Elimu mitindo katika *Uchambuzi wa Matini (Theory of Stylistics)* ilianzishwa na kutumiwa na Jakobson (1960) na Murry (1976). Tunapojishughulisha na uchambuzi wowote wa lugha ya fasihi, jambo la kwanza analokabiliana nalo mtafiti wa maandishi ya aina hiyo ni mtindo kwa upande mmoja na kwa upande mwingine ni elimumitindo katika nadharia ya sanaa ya lugha.

Kihistoria, taaluma ya uchambuzi wa mtindo ilianzia katika kipindi cha karne ya 5 huko Ugiriki na Urumi kabla ya kuzaliwa kwa Masihi. Katika kipindi hiki, balagha au elimu ya usemaji inayohusu ufasaha wa kusema ilikuwa maarufu sana. Taaluma hii ilijumuisha seti za kanuni na mbinu zilizowawezesha wagambi au walumbi na wahutubu (watoaji wa hotuba maalumu) kuzungumza vizuri kwa kutumia lugha iliyopambwa kwa tamathali za semi na taswira kwa lengo la kuleta mabadiliko katika maoni na fikra za hadhira.

Katika nadharia hii, ufundi wa kusema na kuchambua maneno katika kilongo ni njia mwafaka ya kukuwezesha kuwashawishi hadhira wanaokusikiliza ukiwa jukwaani, kanisani au katika kampeni kama za kisiasa. Kwa kuwa njia hii ilikusudiwa

kuwaridhisha au kuwaathiri watu wengine kimaono, tukio la kiisimu lenye sura hiyo lilipata umuhimu wa kiulumbi na bila shaka lilichukuliwa kuwa ni ulumbi wa kielimumitindo. Utafutaji wa athari alizopata msikilizaji inachukuliwa katika nadharia hii kuwa ni kazi ya kiutendaji ya lugha au utendaji hiari unaosababishwa na ujumbe unaopatikana katika kisemo kama alivyosisitiza Jakobson (1960) kwa sababu lugha husababisha mtazamo au mwelekeo na vionjo vya moyo kwa hadhira.

Katika hatua hii ya maendeleo ya taaluma hii Nadharia ya Elimu mitindo katika *Uchambuzi wa Matini* iliweka msisitizo wake katika nafasi ya ujumi wa lugha katika kazi za fasihi. Kwa maneno mengine, lugha ya fasihi iliangaliwa kuwa ilitumia ujumi katika kueneza fikra au ujumbe, ujumi huu ulidhihirishwa katika matumizi ya lugha kisanaa kwa lengo la kuumba wazo na kulisambaza kwa hadhira kwa namna ivutiayo kupita upeo wa matumizi ya lugha ya kawaida.

Kwa hiyo, wachambuzi wa kazi za fasihi waliofuata mwelekeo wa Nadharia ya Elimu mitindo katikaUchambuzi wa Matiniwalielekeza jitihada zao za kifasihi katika vipengele kama vile aina ya lugha iliyotumika, taswira, sitiari na picha kwa lengo la kuchunguza jinsi vipengele hivi vilivyotumika kulipamba au kulirembesha jambo fulani kama lilivyowasilishwa katika kazi ya fasihi inayohusika, hivyo umuhimu ulielekezwa katika uteuzi na upangiliaji wa kisanaa wa maneno katika kazi ya fasihi, huu ni uendelezaji na ukuzaji wa imani kuwa matumizi maalumu ya lugha ni vazi la wazo au fikra.

Nadharia inayozingatia mfumo linganifu katika uchambuzi wa matini za kifasihi haikubaliki kwa mujibu wa nadharia ya Elimumitindo *katika Uchambuzi wa Matini*.

Hivyo, si sahihi kusema kuwa ubadilishaji wa aina yoyote wa mtindo wa kazi ya fasihi utaleta dosari katika kazi hiyo. Wafuasi wa Nadharia ya Elimumitindokatika Uchambuzi wa Matiniwanaamini kuwa kuna mitindo mbalimbali ya kuwasilisha wazo hilo hilo na kwa hiyo katika kazi ya fasihi maudhui na fani ni vitu viwili tofauti.Nadharia hii itatumika kuchambua vipengele mbalimbali vya lugha katika tamthiliya teule.

Sababu za kuteua nadharia hii zimetokana na uwezo wa nadharia na mhimili wa mawazo ya nadharia hii kuwa itaweza kutuongoza katika kuchambua vipengele mbalimbali vya lugha hatimaye kutuwezesha kuibua dhima mbalimbali za kimtindo katika tamthiliya teule. Tumeamua kutumia nadharia hii pia kwa kuzingatia kuwa kila mtunzi wa kazi za fasihi huwa na upekee wake unaoweza kumtofautisha na watunzi wengine hata kama wataandika utanzu mmoja na katika kipindi kimoja. Nadharia hii itafaa kubainisha upekee wa kimtindo baina ya watunzi wa kazi zilizoshughulikiwa katika utafiti linganishi.

## 2.8 Hitimisho

Sura hii imejadili kuhusiana na kazi tangulizi ambayo imeonesha namna ambavyo watafiti wengine walivyofanya utafiti kuhusiana na mambo kadhaa ya kifasihi, ambapo mtafiti alichagua kazi za kiutafiti ambazo zinamwelekeo na kazi ya kiutafiti anayoifanya ili kufahamu nini walifanya, wakagundua nini, wakachambuaje, na tatizo lilikuwa ni nini, pengo la maarifa na hatimaye maarifa gani mapya waliyoyaweka wazi kutumika katika taalimu ya fasihi. Katika sura hii ilianzza na kazi tangulizi katika kuchunguza dhana ya *fasihi linganishi* ambapo wataalamu kama vile wallek (1988), Bassnett (1993) na Guyard kama alivyonukuliwa na Weisstein

(1968) walijadiliwa mawazo yao na kuonekana kipi ambacho hakijafanyika ambacho utafiti huu utakiibua.

Pia katika sura hii mtafiti ametalii kazi tangulizi zinazozungumzia suala la mtindo kwani utafiti wetu unazungumzia dhima ya mtindo, ambapo mtaalamu wa fasihi Senkoro (2011) na Wamitila (2008) walizungumzia dhana ya mtindo kwa mapana ambapo kipengele cha lugha kimegusiwa ambacho ni kipengele muhimu katika utafiti huu. Pia sura hii imeangalia tafiti kuhusu tamthiliya za kiswahili ambapo iligundulika kuwa tafiti nyingi zimefanyika katika kuchunguza fani na maudhui ya kazi hizo, pia tafiti linganishi za msanii wa namna moja.

Kulingana na hayo ikabainika kuwa tafiti linganishi katika kipengele cha mtindo katika tammthiliya za *Morani* na *Kinjeketile* hazijafanyika pia ikihusisha tamthiliya za kihistoria, hivyo kumpatia ari mtafiti kufanya utafiti huu. Pengo la maarifa liliwekwa bayana ambalo ndilo linaloifanya kazi hii ya kiutafiti iweze kufanyika ili kuweka bayana yale ambayo hayakuwa yanafahamika.

Mwisho sura hii iliangalia kiunzi cha nadharia ambapo nadharia ya Elimumtindo katika uchambuzi wa matini ilizungumziwa kuhusu kufaa kwake katika kuchunguza dhima ya mtindo katika tamthiliya teule za utafiti huu. Kulingana na utafiti huu sura hii ni yamuhimu sana kwani humsaidia mtafiti kufahamu nini wengine wamefanya na kipi hakijafanyika ambapo pengo la maarifa litapatikana na kuhimiza utafiti pia nadharia ambayo yaweza kutumika katika utafiti huo maana kama hakuna nadharia inayoweza kufaa utafiti huo utakuwa si wakisayansi.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inajadili mkabala wa utafiti, mbinu, na vifaa ambavyo vilitumika katika utafiti huu. Utafiti huu umetumia mkabala wa kitakwimu na usio wa kitakwimu katika kukusanya na kuzichambua data za utafiti huu. Kama wanavyoeleza (Kombo na Tromp, 2006) kuwa, utafiti wa kitakwimu na usio wa kitakwimu hujazilizana na kukamilishana. Kwa maana hiyo, utafiti huu umehusisha maelezo ya data na pia umetumia nduni za utafiti wa kitakwimu kama vile; matumizi ya namba na asilimia kuelezea matokeo ya data za usaili na dodoso. Hivyo, sura hii inajadili kuhusu mbinu za utafiti na hatua zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika eneo la jiji la Dar es Salaam, ambapo maeneo kadhaa yalichaguliwa na kutumika kulingana na mahitaji ya utafiti huu. Maeneo hayo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo kikuu Huria cha Tanzania na katika shule ya sekondari ya St. Anthon iliyopo Mbagala jijini Dar es Salaam. Sababu za kuchagua maeneo hayo ni kulingana na upatikanaji wa maktaba za kutosha ambapo upatikanaji wa vitabu vilivyotajirisha utafiti huu ulikuwa rahisi, ambapo

Maktaba kuu ya Tanzania hupatikana, maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hupatikana.Sababu nyingine ni eneo ambalo wanafunzi wa fasihi ya kiswahili hususani tamthilya hupatikana, hasa katika

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Huria na wanafunzi wa kidato cha nne wa sekondari ya St. Anthon ambapo wengine husoma kama kozi na wengine kama kitabu cha kiada. Aidha Dar es Salaam ni eneo ambapo wataalamu wengi wa fasihi ya kiswahili hupatikana hususani tamthiliya ya kiswahili ambapo kwa kupitia mawazo yao utafiti huu ulifikia malengo yake.

Dar es Salaam ni eneo ambalo watuzi wa kazi za fasihi zilizotumika katika utafiti huu hupatikana. Katika eneo hili msanii Emmanuel Mbogo hupatikana maana ndiyo makazi yake na hufanya kazi kama Muhadhiri katika Chuo Kikuu Huria na katika eneo hili msanii E.Hussein hupatikana maana ndiyo makazi yake, pia watu wa karibu na watunzi hawa hupatikana katika eneo hili.

## 3.3 Kundi Lengwa

Kulingana na Kothari(2004), Brayman(2004), Komba na Tromp(2006) wanatoa hoja kuwa kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti. Katika utafiti huu kundi lengwa ni watunzi wa kazi zilizotumika katika utafiti huu ambao ni E.Mbogo aliyetunga *Morani* na E.Hussein aliyetunga *Kinjeketile*. Kundi lingine ni waalimu wa fasihi ya kiswahili ambao hutoka Chuo Kikuu Huria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wa shule ya St. Anthon ya Mbagala. Pia kundi lingine ni wanafunzi wa fasihi ya kiswahili katika tamthiliya ambapo wanafunzi St. Anthon na wa Chuo Kikuu Huria na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waliteuliwa ili kukidhi haja ya utafiti huu.

Kundi la mwisho ni watu wa karibu na watunzi wa *morani* na *kinjeketile* ambao wana taarifa za ziada kuhusiana na utendaji kazi zao, lugha wanayotumia na namna

wanavyoandika kazi zao za kifasihi.Zipo sifa mbalimbali ambazo zilisababisha makundi haya kuchaguliwa, tukianza na watunzi wa *Morani* na*Kinjeketile,* hawa ni watu muhimu sana kwani ndio watunzi wa kazi hizo za kisanii na wanaundani wa matumizi ya lugha katika kazi zao, nini kilichowasukuma kuchagua vipengele walivyotumia, hivyo mtafiti hakusita kuwatumia kwani walionekana ni rasilimali ya muhimu katika utafiti huu katika kupata data. Kundi lingine ni watu wa karibu na watunzi, nao ni kundi lengwa la muhimu kwani wanafahamu mengi kuhusiana na watunzi kwani wengine waweza fahamu historia yao, utashi wao, utendaji kazi wao na mitindo wanayotumia katika lugha katika kufikisha ujumbe kwa hadhira.

Kundi lingine ni waalimu wa fasihi ya kiswahili hususani katika tamthilya ya kiswahili, hawa ni kundi muhimu sana kwani wanauzoefu wa kutosha katika kuchambua kazi hizi za kifasihi na kufahamu kanuni za uchambuzi wa kazi za kifasihi. Katika utafiti huu kundi hili lilifanikisha sana kwa kutupatia mawazo yao kuhusu dhima ya kimtindo katika tamthiliya zilizotumika katika utafiti huu. Pia wapo wanafunzi wa fasihi ya kiswahili ambao wanasoma kama kozi inayojitegemea hasa kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu na kama sehemu ya vitabu vya kuchambuliwa katika wanafunzi wa sekondari. Hivyo basi kwa kutumia makundi haya yalifanikisha kupata data ambazo zilitusaidia katika utafiti huu.

### 3.4 Sampuli na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli, kama unavyoelezwa na Bryman (2004), ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwani sio rahisi kutafiti kundi zima. Mchakato wa kuteua sampuli kutoka katika kundi lengwa unajulikana kama mbinu ya uteuzi wa sampuli.

Mbinu yenye madhumuni maalum na dhamira zinahusisha uteuzi wa vitu kama sampuli unaofanywa na mtafiti kwa madhumuni maalum na dhamira kutegemeana na taarifa zinazohitajika kupatikana kwa ajili ya utafiti (Kothari, 1990; Babbie, 1992). Kwa vile siyo rahisi kukusanya taarifa zote kutoka kwenye kundi zima, yaani kundi lengwa, sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu mbili yaani: mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu na na uteuzi rahisi wa sampuli. Sababu ya kuamua kutumia mbinu hizi katika kuteua sampuli ya utafiti huu ilitokana na malengo mahususi ya utafiti huu. Maelezo ya mbinu zilizotumika katika uteuzi wa sampuli ya utafiti huu yanatolewa katika sehemu inayofuata hapa chini:

### 3.4.1 Mbinu ya Uteuzi Rahisi

Mtafiti hakukwepa kutumia mbinu hii katika utafiti huu kwani kwa ujumla mbinu hii haizingatii makusudio maalumu ama kundi fulani ambalo lina sifa maalumu, bali itategemea upatikanaji wa wawatafitiwa. Mbinu hii huruhusu kuchagua mtu yeyote atakayeangukia katika uchaguzi wako, tofauti na mbinu ya madhumuni maalumu ambayo ukichagua waalimu kuwa katika sampuli yako katika kutafuta taarifa inayohusiana na masuala ya kifasihi hautaweza kumchukua mwalimu yoyote hata kama ni wa historia. Kwa kutumia mbinu hii ya uteuzi wa sampuli, mtafiti alichukua orodha ya majina ya wanafunzi wa sekondari. Kwa kutumia orodha hiyo mtafiti aliteua sampuli yake kwa kutumia nafasi kila baada ya mtu wa tano mtafiti aliteua jina la mtu ambaye alilengwa kushiriki kama sampuli yake.

### 3.4.2 Uteuzi wa Madhumuni Maalumu

Mbinu hii imejikita katika kuzingatia sababu maalumu za kwanini sampuli fulani imetumika nah ii ni kutokana na imani aliyonayo mtafiti katika kundi hilo kutokana

na taarifa za awali alizonazo mtafiti kuwa sampuli hiyo ni rasilimali ya muhimu sana katika utafiti huo na ifahamike kuwa ufahamu wa kundi lengwa humrahisishia mtafiti kazi yake. Seale (2012) anasema kwamba ni kutokana na taarifa anazokuwa nazo mtafiti juu ya wahojiwa wake au kwa kuambiwa na watu wa karibu na wahojiwa.

Powell na Connaway (2004) wanasema kuwa katika uteuzi wenye madhumuni maalumu sampuli huteuliwa kwa kuzingatia vigezo ambavyo vinahusiana na maswali ya utafiti kulikoni kigezo cha uteuzi wa nasibu au wa kubahatisha, hivyo wale wanaohojiwa huteuliwa kutokana na nafasi zao kwa imani kwamba ndio rasilimali ya utafiti huu katika kupata data zitakazojitosheleza kukamilisha utafiti. Kulingana na malengo ya utafiti huu, mbinu hii ilionekana kufaa kwani wapo watu walioonekana kufaa kuliko wengine katika kupata data za kiutafiti.

Tukitumia mifano kadhaa kulingana na utafiti wetu waalimu wa kozi ya fasihi katika kipengele cha tamthiliya wakilinganishwa na waalimu wale wasiofundisha tamthiliya walitofautiana sana kulingana na umahiri au ujuzi wao, hivyo kiutafiti lazima uchague wale wenye ujuzi katika fani hiyo na ndivyo katika utafiti huu ilifanyika. Ukilinganisha wanafunzi wa fasihi wanaosoma tamthiliya na wale wasiosoma tamthiliya utaona kuwa wanaofaa kutumiwa ni wale wanaosoma na kuchambua tamthiliya watateuliwa kwa kutumia madhumuni maalumu kwani wanafahamu kanuni za kiuchambuzi na vipengele vya kimtindo ambavyo huhitajiwa.

Kwa ujumla mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu ilifaa kutumika katika utafiti huu kwa kuwa na watu wenye ufahamu na uelewa wa kile kinachohitajika katika

utafiti huu, hivyo mbinu hii ilitumika ikisaidiana na mbinu ya uteuzi rahisi kwani hakuna mbinu moja inayojitosheleza katika kupata taarifa zote zinazohitajika, zote hutegemeana katika kufikia malengo. Kulingana na mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu ilitumika kupata watafitiwa ambao ni waalimu wa fasihi, watunzi wa Morani na Kinjeketile, wanafuzi wanaosoma fasihi kwa chuo kikuu na watu wa karibu na watunzi.Hivyo basi kwa uteuzi huu wa sampuli utafiti huu ulikuwa na jumla ya wahojiwa kama inavyojionesha kwenye Jedwali namba 3.1.

**Jedwali Namba 3.1:Idadi ya Washiriki wa Utafiti**

| Namba | Aina | Jinsia | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Ke | Me | |
| 1. | Wanafunzi wa Chuo Kikuu wanaosoma tamthiliya ya Kiswahili | 10 | 10 | 20 |
| 2. | Wanafunzi wa sekondari (St. Anthon) kidato cha nne wanaosoma kiswahili | 10 | 10 | 20 |
| 3. | Walimu wa fasihi (tamthiliya) Chuo Kikuu Huria na Chuo kikuu cha Dar es Salaam na sekondari ya St. Anthon | 2 | 2 | 4 |
| 4. | Watu wa karibu wa watunzi | 10 | 10 | 20 |
| 5. | Watunzi wa *Morani* na *Kinjeketile* | | 2 | 2 |
| **JUMLA** | | | | **66** |

Chanzo:Utafiti (2014)

Kulingana na Jedwali namba 3.1, utafiti huu utatumia jumla ya wahojiwa 66 ambao walipewa dodoso na kufanyiwa usaili.

### 3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Katika utafiti, mbinu mbalimbali huweza kutumika katika ukusanyaji wa data kama Seale (2012) na Silvaman (2010) wanavyounga mkono hoja kuwa zipo mbinu

mbalimbali za kukusanya data na mbinu hizo hakuna ambayo inajitosheleza katika mazingira yote hivyo kutegemeana katika kupata data zilizo bora. Ukweli kuwa zipo mbinu mbalimbali za ukusanyaji wa data, mtafiti asingeweza kutumia zote bali katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu tatu ambazo ni mbinu ya dodoso, usaili na mbinu ya usomaji wa maktabani na hakuna ambayo ilijitosheleza bali kila mbinu ilichangia kufikia malengo ya kiutafiti.

### 3.5.1 Mbinu ya Dodoso

Mbinu hii hutumiwa na watafiti kwa kuandaa dodoso ambalo linakuwa na maswali yaliyoko katika mpangilio maalumu ambapo hutumwa kwa mhusika ambaye atatakiwa kujibu maswali hayo na kuyarudisha kwa mtafiti kwa njia ambayo ataelekezwa kuitumia. Mbinu hii huungwa mkono na Kothari (2004) akisema kuwa mbinu hii huhusisha uandaaji wa dodoso ambalo hutumwa kwa mhusika na ombi la kujibu maswali yaliyomo katika dodoso hilo na hatimaye kurudishakwa mtafiti.

Ni wajibu wa mtafiti kuandaa maswali mengi ambayo anafikiri yakijibiwa atapata data za kukidhi utafiti husika. Mara nyingi dodoso laweza tumwa kwa posta ama kwa kupitia wasaidizi wa mtafiti mkono kwa mkono, ambapo kama ni kwa posta mtafiti anaweza kuweka stempu ndani ya bahasha ya dodoso ili kumrahisishia mtafitiwa wakati wa kutuma majibu ya dodoso. Sababu ya kutumia mbinu hii ni kwakuwa mhojiwa huwa huru kuelezea hisia, mawazo na maoni yake juu ya yale aliyoulizwa.

Mbinu hii ilitufaa sana katika utafiti huu kwani wanafunzi 10 wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, wanafunzi 10 wa St.Anthon,

waalimu 2 wa tamthiliya, watu 10 wa karibu na watunzi na watunzi 2 walipewa dodoso, ambapo kulingana na mwitikio wao data zao zilineemesha utafiti huu. Changamoto aliyokabiliana nayo mtafiti ni baaadhi ya vipengele kutojibiwa na kukosa majibu sahihi ya kile kilichokuwa kinatarajiwa. Hivyo mtafiti alilazimika kutumia mbinu nyingine ili kutatua tatizo hilo.

### 3.5.2 Mbinu ya Usaili

Mbinu hii inahusisha mawasiliano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na mtafitiwa ama wahojiwa ambapo mtafiti huweza andaa maswali ya mwongozo katika mazungumzo ili kufikia lengo lake. Kupitia mbinu hii mtafiti anaweza kupata taarifa za ziada ambazo kwa kutumia dodoso asingeweza kuzipata kwani hata mtafiti anaweza kubadili mpangilio wake wa mazungumzo ili kufikia lengo. Babbie (1992) anaunga mkono hoja hii akisema usaili lazima uhusishe mawasiliano ya moja kwa moja baina ya mtafiti na mhojiwa na mtafiti hupata maelezo ya ziada kuhusu baadhi ya mambo ambayo yasingeweza kuwekwa bayana kupitia mbinu nyingine ya utafiti. Kupitia mbinu hii inawezesha unyumbukaji wakati wa kuuliza maswali na kutaka ufafanuzi kwa vipengele ambavyo vinaonekana kutokuwa wazi.

Ni dhahiri kuwa mbinu hii ilifaa sana katika utafiti huu kwani data zake zilionesha ubora na ufanisi. Mbinu hii ilitumika katika data ili kujalizia kile ambacho mbinu ya dodoso isingeweza kutupatia, ikifahamika kuwa kila mbinu inamatatizo yake. Wanafunzi 10 wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, wanafunzi 10 wa St.Anthon wa kidato cha nne, waalimu 2 wa tamthiliya Chuo Kikuu na Sekondari, watu 10 wa karibu na watunzi na watunzi 2 walifanyiwa usaili ili kupata data za kutosha ili kuunganisha na zile za dodoso.

### 3.5.3 Mbinu ya Usomaji wa Maktabani

Mbinu ya usomaji wa maktabani huhusisha kutafuta data kwa kusoma vitabu mbalimbali kama vile vitabu teule, tahakiki, majarida, na vitabu vya ziada kulingana na malengo ya utafiti ili kupata data zitakazo kidhi haja ya kiutafiti. Mbinu hii ilitumika katika utafiti huu ambapo mtafiti alisoma na kuchambua vitabu vya *Morani* na *Kinjeketile* pamoja na vitabu vingine vya ziada ambavyo viliwezesha kupata taarifa za muhimu katika utafiti huu.

Kwa kusoma vitabu hivyo vilivyopatikana katika maktaba mtafiti aliweka bayana vipengele vya kimtindo katika tamthiliya zote na hivyo kuweza kugundua namna vinavyotofautiana na kufanana na namna ambavyo mtindo katika lugha hufikishia ujumbe katika kazi ya kifasihi. Mbinu hii ni bora kwani maktabani unaweza kupata vitabu na majarida yanayozungumzia kile unachotafiti na pia kupata mawazo ya ziada kuhusiana na wengile walivyoshughulikia tatizo hilo.

Mbinu hii ilifaa sana katika utafiti huu ingawa isingeweza kujitosheleza kwani yapo mambo mengine kama ya hisia za mtunzi ambazo usingeweza kuzipata katika maandishi, hivyo mbinu hii ilisaidiana na mbinu ya dodoso na usaili ili kupata data za kutosha za kiutafiti. Watunzi wa *Morani* na *Kinjeketile* wao walipewa dodoso na kufanyiwa usaili kwani ilionekana dodoso tu lisingetosha na wasaidizi walihusika katika kugawa dodoso na kufanya usaili kwani walionekana kuwa na ujuzi wa mbinu zote mbili hivyo kurahisisha zoezi la ukusanyaji wa data.

## 3.6 Zana za Utafiti

Kubuk (1987) anasisitizia juu ya kutumia zana za tafiti, ambazo ni za muhimu sana kwa mtafiti ambazo ni kalamu na daftari kwa ajili ya kuandikia na kutunzia

kumbukumbu muhimu, zitakazopatikana wakati wa mahojiano, usaili na majadiliano. Zipo zana nyingi za kiutafiti ila tutazungumzia chache zilizotumika sababu ya malengo ya utafiti huu, zifuatazo ni zana ambazo mtafiti amezitumia wakati kukusanya data katika utafiti huu:

### 3.6.1 Mwongozo wa Usaili

Mwongozo wa usaili ni mojawapo ya zana ambayo mtafiti ametumia ambapo aliandaa maswali ya usaili kwa ajili ya wahojiwa ili kupata data za kiutafiti. Katika utafiti huu mwongozo wa usaili ulitumika na kusaidia kukusanya data ambazo zilifanikisha kazi hii.

### 3.6.2 Matini

Vipo vitabu ambavyo vimetumika katika utafiti huu kwa ajili ya kuchunguza na kubainisha dhima ya mtindo ambavyo ni Morani na Kinjeketile pamoja na vitabu vingine kama vya kiuhakiki ambapo matini hizi zilitoa mchango mkubwa katika utafiti huu kwani data za kimtindo zilipatikana na kufanikisha utafiti huu.

### 3.6.3 Dodoso

Katika utafiti huu dodoso ni mojawapo ya zana za kiutafiti zilizotumiaka ambapo dodoso kadhaa ziliandaliwa na kutumwa kwa wahojiwa ili kupata data zilizokuwa zinahitajiwa katika utafiti huu na kwakupitia zana ya dodoso mtafiti alipata data zilizo makini ambazo zimesababisha utafiti huu kuwa bora sana.

### 3.6.4 Kinasa Sauti

Matumizi ya umakini ya zana hii wakati wa kukusanya data huitajirisha kazi ya kiutafiti kwani wakati wa usaili au wakati wa mahojiano haiwezekani kuandika kila

kitu kinachozungumzwa na mtafitiwa, hivyo ili kumsaidia mtafiti kurejelea hoja za msingi alizosahau wakati wa kuchukua taarifa hurekodi kwa kutumia kinasa sauti ambapo akiwa ametulia anaweza kufungulia sauti na akapata taarifa za ziada ambazo hakuziandika, pia husaidia kuwa na kumbukumbu hasa katika vipengele vya toni na hisia.

### 3.7 Uchambuzi wa Data

Data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu mbili, ambazo ni *uchambuzi linganishi* na *uchambuzi maudhui,* japo tukifahamu kuwa zipo mbinu nyingine ambazo zinaweza kutumika katika kuchambua data za utafiti wa namna hii, pia tukiweka bayana kuwa utafiti huu una sifa za utafiti usio wa kitakwimu na utafiti wa kitakwimu. Katika uchambuzi mtaalamu Tromp (2006) anaelezea kuwa uchambuzi maudhui ni mbinu ya uchambuzi ambayo huziweka mada kulingana na jinsi zinavyofanana na kuhusiana ambapo dhamira zilizobainishwa huwekwa pamoja kukidhi haja ya kiutafsiri wa data.

Katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu hii kwani aliona itamfaa katika kufikia malengo yake ambapo uchambuzi maudhui ulimsaidia kupata maudhui katika kazi zote mbili za kiusanii na kuona namna gani vipengele vya mtindo vilivyo nadhima kubwa katika kuelezea maudhui, pia kuweka bayana suala la kihistoria ambalo linawekwa bayana kupitia maudhui. Uchambuzi linganishi ni mbinua mbayo mtafiti ametumia katika utafiti huu katika kulinganisha data kutoka katika vyanzo mbalimbali kama kutoka kwa watunzi, wanafunzi wa sekondari, wanafunzi wa chuo kikuu na kutoka kwa watu wa karibu na watunzi, pia kutoka katika mbinu za ukusanyaji wa data. Mbinu hii ilitumika ili kulinganisha vipengele vya lugha katika

tamthiliya za *Morani* na *Kinjeketile* ili kupata majumuisho ya namna ambavyo vipengele vya kimtindo vilivyotumika na wasanii hao. Katika utafiti huu mtafiti alifanya yafuatayo katika uchambuzi wa data:

(1) Kuchambua vipengele vya lugha katika tamthilia za *Morani* na *Kinjeketile*

(2) Kuchambua dhima ya vipengele vya kimtindo katika tamthiliya za *Morani* na *Kinjeketile*

(3) Kulinganisha na kutofautisha vipengele vya lugha katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjekitile*

(4) Kutafsiri matokeo ya dodoso, usaili na usomaji wa maktaba na kuweka majibu yanayofanana na kuhusiana katika kundi moja

(5) Kuchambua na kuzitafsiri data za usaili, dodoso na maktaba na kuzijadili kwa kutumia namba na maelezo.

## 3.8 Hitimisho

Sura hii imejadili juu ya mbinu za utafiti ambapo eneo la utafiti lilibainishwa, kundi lengwa, sampuli na mbinu za uteuzi wa sampuli, mbinu za ukusanyaji wa data, zana za utafiti na uchambuzi wa data. Aidha katika kundi lengwa tunaona umuhimu wa walengwa ambao wametumika katika kutupatia data zilizotufaa katika utafiti huu wakiwepo watunzi wa vitabu vya Morani na Kinjeketile, watu wakaribu na mtunzi na waalimu ambao wanafahamu kanuni za uchambuzi wa kazi za kifasihi na wanafunzi wanaosoma kozi hiyo. Sampuli iliyotumika ilizingatia uteuzi wa madhumuni maalumu na uteuzi rahisi kwani mtafiti aliona kuwa mbinu moja ya uteuzi wa sampuli haiwezi kujitosheleza. Katika ukusanyaji wa data mbinu ya usomaji wa maktaba ilitumika kiufanisi na mbinu ya usaili na dodoso zilitumika nah

ii ni kutokana na kwamba mbinu hizi zinategemeana katika kupata taarifa za kidata ambazo ziko makini. Mtafiti pia alionesha namna gani zana za utafiti zilivyo na umuhimu na jinsi zinavyotegemeana kasha kufanikisha katika uchambuzi wa data kwa kutumia mbinu mbili ambazo ni uchambuzi maudhui na uchambuzi linganishi.

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data zilizokusanywa katika utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nne; sehemu ya kwanza inahusu vipengele vya lugha katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile*, sehemu ya pili inajadili juu ya dhima ya vipengele vya lugha katika *Morani* na *Kinjeketile*, sehemu ya tatau inahusu kulinganisha na kulinganua matumizi ya vipengele vya lugha katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile* na Sehemu ya mwisho ni hitimisho.

## 4.2 Vipengele vya Lugha katika Tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile*

Moja ya malengo mahususi ya utafiti huu ilikuwa ni kubainisha vipengele vya lugha katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile* japo tutatumia vipengele vichache tu katika kuvichambua ili kufikia malengo ya utafiti huu, ambavyo ni tamathali za semi na si vipengele vyote vya lugha katika mtindo. Ili kufikia lengo hilo, utafiti huu ulitumia mbinu ya usomaji wa machapisho kusoma na kuchambua tamthiliya hizo ili kuweza kubaini vipengele vya lugha katika tanmthiliya hizo.

Aidha data kutoka katika dodoso, usaili na majadiliano ya vikundi zilitumika ili kujaziliza data zilizopatikana katika mapitio ya maandiko. Utafiti huu ulibainisha vipengele vya lugha vilivyotumika katika tamthiliya hizo kama ifuatavyo. Matokeo ya utafiti yalikuwa kama inavyojidhihirisha katika jedwali lifuatalo:

Jedwali namba 4.1 hapo juu, linaonyesha vipengele vya lugha ambavyo vilijitokeza katika tamthiliya ya *Morani*.

**Jedwali Namba 4.1:Vipengele vya Lugha katika *Morani***

| Namba | Kipengele cha Lugha |
|---|---|
| 1. | Tamathali za semi |
| 2. | Misemo |
| 3. | Nahau |
| 4. | Methali |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Morani* (2014)

Data za utafiti huu zinadhihirsha kuwa msanii wa *Morani* ametumia tamathali za semi, misemo, nahau na methali katika ujenzi wa kazi yake ya fasihi, na kwa upande mwingine, utafiti huu ulibainisha vipengele vya lugha vinavyojitokeza katika tamthiliya ya *Kenjikitile*. Matokeo yalikuwa kama yanavyojidhihirisha katika Jedwali Namba 4.2.

**Jedwali Namba 4.2:Vipengele vya Lugha katika Kinjeketile**

| Namba | Kipengele cha Lugha |
|---|---|
| 1. | Tamathali za semi |
| 2. | Misemo |
| 3. | Methali |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Kenjeketile* (2014)

Jedwali Namba 4.2 hapo juu linaonyesha vipengele vya lugha ambavyo vimejitokeza katika tamthiliya ya *Kinjeketile*, kama ilivyokuwa katika *Morani*, utafiti huu ulibaini kuwa msanii wa *Kinjeketile* ametumia vipengele vya lugha kama vile; tamathali za semi, misemo, na methali katika ujenzi wa kazi yake ya fasihi. Aidha tofauti na

*Morani,* katika *Kinjeketile* msanii hajatumia nahau wakati kipengele hiki kimejitokeza sana katika tamthiliya ya Morani. Hata hivyo utafiti huu ulichunguza mawanda ya utumizi wa vipengele hivyo katika kila tamthiliya na kiwango cha ujitokezaji wa vipengele hivyo vya lugha. Lengo lilikuwa ni kufanya ulinganishi wa matumizi ya vipengele hivyo katika tamthiliya hizo. Matokeo yalikuwa kama yanavyowasilishwa katika Jedwali namba 4.3 na 4.4 katika sehemu inayofuata.

## 4.3 Mdafao wa Ujitokezaji wa Vipengele vya Lugha katikaTamthiliya Teule

Utafiti huu ulichunguza mdafao wa ujitokezaji wa vipengele vya lugha katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile*. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:

**Jedwali Namba 4.3:Mdafao wa Utokeaji wa Vipengele vya Lugha Katika *Morani***

| Namba | Kipengele cha Lugha | Mdafao wa ujitokezaji |
|---|---|---|
| 1. | Tamathali za semi | 88% |
| 2. | Misemo | 3% |
| 3. | Nahau | 2% |
| 4. | Methali | 7% |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Morani* (2014)

Jedwali Namba 4.3 linawasilisha mdafao wa ujitokezaji wa vipengele vya lugha katika tamthiliya ya *Morani*. Data inadhihirisha kuwa mtunzi ametumia tamathali za semi kwa asilimia 88 wakati vipengele vingine vinajitokeza kwa asilimia zilizobaki. Matokeo haya hayakutofautiana na matokeo ya *Kinjeketile* ingawa wahojiwa walibainisha kuwa mtunzi wa tamthiliya ya *Kinjeketile* katumia lugha ya kawaida

isiyokuwa na ugumu wa kumfanya msomaji atafute maana halisi ya kazi ya sanaa. Tazama Jedwali 4.4.

**Jedwali Namba 4.4:Mdafao wa Ujitokezaji wa Vipengele vya Lugha katika Kinjeketile**

| Namba | Kipengele cha Lugha | Mdafao wa Ujitokezaji |
|---|---|---|
| 1. | Tamathali za semi | 90% |
| 2. | Misemo | 5% |
| 3. | Methali | 5% |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Kenjeketil* (2014)

Jedwali Namba 4.4 linawasilisha mdafao wa ujitokezaji wa vipengele vya lugha katika tamthiliya ya Kinjeketile. Data indhaihirisha kuwa mtunzi ametumia tamathali za semi kwa asilimia 90 ukilinganisha na vipengele vingine vya lugha. Baada ya kubainisha vipengele vya lugha katika tamthiliya teule, utafiti huu ulichunguza ni kwa kiasi hani vipengele hivyo vinajitokeza katika tamthiliya moja na jinsi gani ujitokezaji wake unatofautiana na tamthiliya nyingine. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:

## 4.4 Uteuzi na Matumizi ya Tamathali za Usemi

Tamathali za usemi ni maneno au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata sauti katika maandihsi ama kusema (Senkoro, 2011). Ni usemi wenye kupanua, kupunguza au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu ya kishairi iliyokusudiwa na mtunzi (Kahigi na Mulokozi, 1979). Tamathali hizi za usemi ni kama ifuatavyo:

**Jedwali Namba 4.5:Tamathali za Usemi Katika Tamthiliya ya *Morani***

| Namba | Tamathali ya semi |
|---|---|
| 1. | Sitiari |
| 2. | Tashibiha |
| 3. | Tashihisi |
| 4. | Takriri |

Chanzo: Data kutoka katika *Morani* (2014)

Jedwali namba 4.5 hapo juu linaonyesha tamathali za usemi ambazo zimejitokeza katika tamthiliya ya *Morani*. Utafiti huu ulichunguza ni kwa kiwango gani kila tamathali ya semi imetumika katika tamthiliya ya *Morani*. Lengo lilikuwa ni kujua ni tamathali gani inatumiwa mara nyingi zaidi na msanii katika kujenga kazi yake ya fasihi. Kwa kufanya hivi pia tuliweza kubaini sifa ya kimtindo ya msanii katika uteuzi wa tamathali za usemi. Matokeo yalikuwa kama kama yanavyojionesha katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Namba 4.6:Mdafao wa Ujitokezaji wa Tamathali za Usemi katika Morani**

| Namba | Tamathali ya Semi | Mdafao wa Ujitokezaji |
|---|---|---|
| 1. | Sitiari | 75 |
| 2. | Tashibiha | 12 |
| 3. | Tashihisi | 9 |
| 4. | Takriri | 6 |
| **Jumla** | | **102** |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Morani* (2014)

Matokeo katika jedwali namba 4.6 hapo juu ambalo halikutumia kigezo cha asilimia, yanaonesha kuwa, sitiari ndiyo tamathali ya usemi ambayo imejitokeza kwa kiasi kikubwa. Sitiari imeonekana kuwa na mdafao wa 75 ikifuatiwa na tashibiha 12,

tashihisi 9 na takriri 6. Hii inadhihirisha kuwa, msanii ametumia sitiari kwa kiwango kikubwa katika kujenga maudhui ya kazi yake. Sehemu ifuatayo inajadili kwa kina kuhusu tamathali za semi zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Morani*.

**4.4.1 Sitiari**

Utafiti huu ulibaini kuwa msanii wa tamthiliya ya *Morani* ametumia sitiari. Katika *Morani*, sitiari imetumika kwa kiwango kikubwa na ndiyo inayobeba maudhui ya tamthiliya hii. Ilielezwa na wahojiwa wakati wa majadiliano ya vikundi kuwa *Morani* ni tamthiliya iliyobuniwa kisanii kwa sitiari ili kuwasilisha dhana ya hali ngumu ya maisha na harakati za ujenzi wa jamii mpya. Sitiari ni tamathali ya usemi inayotumika kuumba picha fulani inayotoa athari fulani au inayoamsha mwitikio fulani kutoka kwa hadhira (Mulokozi, 2002). Ni uhamishaji wa maana toka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine. Vikao vya maana vinavyohusika katika uhamishaji huu huwa vinatofautiana angalau kwa sifa ya kisemantiki moja ya msingi. Kinachohamishwa ni tabia au umbo au kazi ya kitu kwa kuhusisha na tabia au umbo au kazi ya kitu kingine (Kahigi, 1995).

Katika morani, utafiti huu umebaini kuwa sitiari iliyotumika ni sitiari pana ambavyo inajengwa na tamathali zingine za usemi kama vile tashibiha, takriri na tashihisi. Suala la sitiari pana limezungumziwa pia na Jilala (2008) katika uchunguzi wake wa nyimbo za kizazi kipya ambapo aligundua kuwa nyimbo za kizazi kipya zinajengwa na sitiari pana.

Jedwali Namba 4.7 linawasilisha baadhi ya sitiari ambazo zilibainishwa katika tamthiliya ya *Morani.*

**Jedwali Namba 4.7:Mifano ya Sitiari katika *Morani***

| **Namba** | **Sitiari** |
|---|---|
| 1. | Udongo |
| 2. | Dongo |
| 3. | Dege shaba |
| 4. | Machozi ya damu |
| 5. | Mizuka |
| 6. | Ndimu |
| 7. | Lazima niwafumbue macho |
| 8. | Bwnaa mizuka |
| 9. | Jabali |
| 10. | Dongo likawa mbolea ya shamba lake |
| 11. | Jeneza/ kaburi mapambano yanaendelea |
| 12. | Watu wana macho lakini yamefunikwa na kaniki |
| 13. | Masikio yao yamezibwa kwa nta hawawezi kusikia sauti ya kucha kuchele |
| 14. | Sauti |
| 15. | Maua |
| 16. | Magugu |
| 17. | Safari |
| 18. | Nguzo ya uswezi |
| 19. | Uswezi |
| 20. | Neno |
| 21. | Udongo tasa |

| | |
|---|---|
| 22. | Joho jeupe |
| 23. | Mzizi |
| 24. | Wembe |
| 25. | Tembo |
| 26. | Umeota meno jana unajua nini umekua |
| 27. | Bundi |
| 28. | Sauti zenye harufu kali |
| 29. | Joto |
| 30. | Kivuli |
| 31. | Kama wewe umenunuliwa siyo mimi |
| 32. | Ndimi za moto zipendazo kuivisha vyakula haziwezi kugombana na maji |
| 33. | Hatuwezi kuwaacha mapapa tukavua pelage |
| 34. | Mimi sina uhakika juu ya mpaka |
| 35. | Mkuyu |
| 36. | Hewa yake ni chachu mno |
| 37 | Hasa matunda yake yakidondoka chini hewa yake huwa chachu hupeperushwa na kuingia hapa ofisini |
| 38. | Baada ya muda hujisikia kama nimelewa |
| 39. | Watoto wangevutiwa na sanaa ya utundu kabla ya tamaa ya njaa, kitu aghalabu, |
| 40. | Katika mvuto na uzuri wa kila tunda umeficha funza wadogo wadogo wasioonekana kwa urahisi |
| 41 | Sizungumzii undugu wa damu ila wa kalamu |
| 42. | La sivyo tutajikuta tumetumbukiza mikono yetu katika |

| | |
|---|---|
| | mafuta yanayotokota |
| 43. | Mnataka damu imwagike |
| 44. | Haya tapika |
| 45. | Baba akikomba mboga anaweza akasingizia mtoto. Tunaweza kunawa kwa njia hiyo |
| 46. | Hana lolote huyu |
| 47. | Aidha unamuua chui au unaacha kujitumbukiza katika harakati za uwindaji. Ukimjeruhi ukamwacha damu ikamvuja basi ujue umekwi |
| 48. | Paka |
| 49. | Panya |
| 50. | Kuku |
| 51. | Ushanga mwekundu |
| 52. | Hatua yetu haitakanyaga bali itauzima moto |
| 53. | Vinyonga wawili wanakuja |
| 54. | Nakwambia Mlemeta kama hii ni vita |
| 55. | Tutapumzikaje wakati miti yote imepukutika |
| 56. | Tutapumzikaje wakati telemkatukaze za wanyonge zimejaa kunguni na papasi? |
| 57. | Huu ni wakati wa kunoa mashoka |
| 58. | Nitawatuma matarishi, madereva na wafagia vyoo waungôe na kiteketeza mizizi yake |
| 59. | Umechuma mali hii |
| 60. | Au niende nje ya nchi nikae huko hadi joto lipungue |
| 61. | Madola yao yote yamechukuliwa mastoo yao yote yalikuwa |

| | |
|---|---|
| | yamejaa |
| 62. | Nenda ukamwambie huyo Kinyozi kuwa magogo hayana nywele yana vipara. |
| 63. | We moto |
| 64. | Nani akavimbe |
| 65. | Wenzako wako ngomeni zamu yako imefika |
| 66. | Wote ni mayai ya kuatamiwa, kesho makinda, kesho kutwa labda ndipo mwote mbawa, mnajua tumeitoa wapi nchi hii |
| 67. | Kuchuma madola |
| 68. | Bado u binti mbichi |
| 69. | Fedha yake nyembamba |
| 70. | Nani anataka fedha yako iyonuka damu |
| 71. | Lakini aliniambia hawezi kujificha na kusaliti umma wakati huu wa damu |
| 72. | Risala yenye mishale ya sumu. Sumu itakayounguza maini na mapafu ya wahujumu uchumi, mabepari, mabepari uchwara, vibaraka na vibaraka popote walipo |
| 73. | Watu hawa wanaotambaa kwa magoti, mikononi wameshika vijinga vya moto ili kuitafuta njia |
| 74. | Ndege na papa wa dhahabu wako hewani na majini |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Morani* (2014)

Mifano ya sitiari katika Jedwali Namba 4.7 inadhihrisha kuwa msanii wa *Morani* ametumia sitiari kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na tamathali zingine za semi. Sitiari hizi zimetumika kujenga dhamira za tamthiliya ya *Morani*, Kwa mfano katika mfano namba 38 msanii anatumia sitiari ópakaô kurejelea watumishi wa serikali ambao ni wasaliti na mfano namba 39 msanii katumia sitiari ópanyaô kurejelea

wahujumu uchumi. Aidha, katika mfano namba 48, msanii anatumia sitiari óHuu ni wakati wa kunoa mashokaô kujenga dhana ya vita dhidi ya wahujumu uchumi ili kujikomboa kiuchumi, hivyo basi, sitiari zilizotumika katika tamthiliya ya *Morani* zimetumika kujenga dhamira za tamthiliya hii.

### 4.4.2 Tashibiha

Ni tamathali ya usemi inayotoa mfano wa vitu unaojengwa kwa maneno kwa kulinganisha vitu viwili au zaidi kwa kutumia vilinganishaji, kama, mithili ya na kadhalika (Mulokozi, 2002; Kahigi, 1995; Senkoro, 1982). Hivyo basi, kwa kutumia fasili hiyo, utafiti huu ulichunguza na kubainisha tashibiha zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Morani* kama ifuatavyo:

**Jedwali Namba 4.8:Tashibiha katika *Morani***

| **Namba** | **Tashibiha katika *Morani*** |
|---|---|
| 1. | Inabidi aendelee kuelea angani kama kishada |
| 2. | Nungunungu na mlemeta ni kama kupe na mkia wa ngôombe |
| 3. | Wana akili kuzidi watu kama wewe Yusufu |
| 4. | Unazungumza kama mchawi |
| 5. | Unalia bila sababu kama mtoto vile |
| 6. | Unaniweka mi saa zote pale nyumbani ka askari jela |
| 7. | Hii kampeni mmeivaa tu kama koti la kutungua |
| 8. | Tutawasambaza kama punje za mtama |
| 9. | Watu wengi kama sisimizi |
| 10. | Mizuka iliyokongoroka mifupa, nywele zilizotimka, ngozi zao kama gamba la nyoka |
| 11. | Hakuna kiumbe kishangiliacho pamabazuko la jua kama jogoo |
| 12. | Wachawi rangi zao kama kinyonga |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Morani* (2014)

Jedwali Namba 4.8, linawasilisha tashibiha zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Morani,* katika tamthiliya hii msanii ametumia tashibiha kuwasilisha maudhui ya kazi yake ya fasihi. Kwa mfano, katika mfano namba 7 msanii analinganisha kampeni ya kukamata wahujumu uchumi na koti la kutungua. Koti la kutungua ina sifa ya kutomtosha mvaaji wa koti hilo, kuwa kubwa ama dogo.

Hivyo, matatizo, vikwazo na ugumu wa kutekeleza kampeni ya kuwaondoa wahujumu uchumi yanalinganishwa na koti la kutungua. Aidha, katika mfano namba 12 ówachawi hubadilika kama kinyongaô katika mfano huu, msanii anatumia tashibiha hiyo kuwasilisha suala la usaliti kwa viongozi na watekelezaji wa sera za nchi. Msanii anawafananisha viongozi hao na kinyonga ambaye hubadilika na kugeuka.

**4.4.3 Tashihisi**

Utafiti huu ulibaini kuwa msanii wa *Morani* ametumia tashihisi kuwasilisha maudhui ya kazi yake. Senkoro (1982) anafasili tashihisi kuwa ni tamathali ya usemi ambayo wakati mwingine huitwa tamathali ya binadamu. Kwa tamathali hii vitu visivyo na sifa walizonazo watu hupewa sifa hizo. Mfano nyota zilikuwa zikitabasamu huku zimemzunguka mama yao, jedwali lifuatalo linawasilisha baadhi ya tamathali za semi zilizobainishwa katika tamthiliya ya *Morani.*

Jedwali namba 4.9 hapo juu linaonyesha tashihisi zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Morani.*Tashihisi hizi zinadhihirisha kuwa msanii ametumia ubunifu kujenga maudhui ya kazi yake ya sanaa. Kwa mfano, katika mfano namba 3 anasema ómito ikalowana kwa simanziô hapa msanii kaipa uhai mito kwa kuipa sifa ya kuwa na simanzi, sifa ya kuwa na simanzi ni sifa ya binadamu.

**Jedwali Namba 4.9:Mifano ya Tashihisi katika *Morani***

| Namba | Tashihisi |
|---|---|
| 1. | Jua likajibanza mawinguni |
| 2. | Mwezi ukageuka damu na nyota zikafinya |
| 3. | Mitoé ikalowana kwa simanzi |
| 4. | Dunia ilisimama |
| 5. | Dongo lile lilisimama likasafiri safari ndefu likitafuta chakula |
| 6. | Neno litatuonyesha wapi walikoficha nguzo ya uswezi |
| 7. | Nyota ilinguruma niifuate |
| 8. | Joho jeupe liliota mbawa |
| 9. | Nundu zake muviringo hutema mate machungu yenye sumu yayeyushayo miamba |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Morani* (2014)

Hivyo kwa kutumia tashihisi hii msanii anajenga maudhui ya hali ngumu ya uchumi katika jamii na jinsi jamii ilivyoathirika na umaskini. Aidha, sambamba na hiyo mfano namba 3 unasema ódunia ilisimamaô kwa kutumia tashihisi hii msanii anaipa uhai dunia kuwa na uwezo wa kusimama tendo ambalo linaweza kufanywa na binadamu na viumbe vyenye uhai. Aidha, kwa kutumia tashihisi hii msanii anawasilisha dhana ya umaskini katika jamii.

### 4.4.4 Takriri

Utafiti huu ulibaini kuwa msanii wa *Morani* ametumia takriri katika kujenga maudhui ya kazi yake. Jedwali namba 4.10 linawasilisha mifano ya takriri iliyotumika katika tamthiliya ya *Morani*

**Jedwali Namba 4.10:Matumizi ya Takriri katika *Morani***

| Namba | Takriri |
|---|---|
| 1. | Bundi! Bundi! Bundi |
| 2. | Funga funga |
| 3. | Ugomvi ugomvi |
| 4. | Tutapambana tutapambana |
| 5. | Tulia tulia |
| 6. | Wananicheka nini! wananicheka nini |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Morani*, Juni, 2014

Jedwali namba 4.10 hapo juu linawasilisha baadhi ya takriri ambazo zimetumika katika tamthiliya ya *Morani*, msanii ametumia takriri kuwasilisha ujumbe alioukusudia kwa jamii. Kwa mfano, msanii anatumia Bundi! Bundi! Bundi! Kusisitiza juu ya suala la usaliti na uovu katika jamii. Bundi kama ndege katika jamii za Kiafrika hususani za Tanzania huaminika kuwa ni ndege ambaye sauti yake inaposikiks huashiria jambo baya kama vile kifo. Hivyo uradidi wa sauti ya Bundi unawasilisha suala la usaliti na uovu katika harakati za kupambana na wahujumu uchumi.

## 4.5 Matumizi ya Tamathali za Semi katika *Kinjeketile*

Utafiti huu ulichunguza tamathali za semi katika tamthiliya ya *Kinjeketile* na kubaini kuwa mtunzi wa tamthiliya hii ametumia tamathali za semi japo kwa kiasi kidogo. Katika uwasilishaji wa maudhui ya kazi yake ametumia lugha rahisi na yenye kueleweka kwa kuweka wazi maudhui anayoyawasilisha. Tofauti na *Morani* ambayo mtunzi ametumia zaidi sitiari kuwasilisha maudhui ya kazi yake, pamoja na ugunduzi huo baadhi ya tamathali za semi zilizobainika ni kama ifuatavyo:

## 4.6 Tamathali za Semi

Tamathali za semi zilizobainishwa katika tamthiliya ya *kinjeketile* ni; sitiari, tashibiha, tashihisi na takriri. Aidha, baada ya kubainisha tamathali za semi, utafiti huu ulichunguza ni kwa kiwango gani kila tamathali ya semi imetumika katika tamthiliya hiyo lengo lilikuwa ni kubaini tamathali inayotumiwa mara nyingi zaidi. Matokeo yalikuwa kama yanavyojionesha katika jedwali lifuatalo hapa chini;

**Jedwali Namba 4.11:Mdafao wa Ujitokezaji wa Tamathali za Semi katika Kinjeketile**

| Namba | Tamathali ya Semi | Mdafao wa Ujitokezaji |
|---|---|---|
| 1. | Takriri | 24 |
| 2. | Sitiari | 30 |
| 3. | Tashihisi | 1 |
| 4. | Tashibiha | 6 |
| **Jumla** | | **61** |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Kinjeketile* (2014)

Matokeo katika Jedwali namba 4.11, yanaonesha kuwa sitiari ndiyo tamathali ya usemi ambayo imejitokeza kwa kiasi kikubwa. Matokeo haya hayakutofautiana na matokeo yaliyopatikana wakati wa majadiliano ya vikundi ambapo wahojiwa walieleza kuwa msanii ametumia sitiari ili kuweka msisitizo wa suala la harakati za ukombozi. Hivyo basi, utafiti huu ulibaini kuwa sitiari imetumika kama mbinu ya kuweka msisitizo katika suala nyeti la harakati za jamii kutaka kujikomboa kutoka katika mikono ya wakoloni.

### 4.6.1 Sitiari

Utafiti huu uligundua kuwa msanii wa *Kinjeketile* ametumia sitiari katika kujenga maudhui ya kazi yake. Zifuatazo ni baadhi ya sitiari ambazo zilibainishwa katika tamthiliya ya *Kinjeketile*:

**Jedwali Namba 4.12:Matumizi ya Sitiari katika *Kinjeketile***

| **Namba** | **Sitiari** |
|---|---|
| 1. | Nyoka |
| 2. | Udongo mwekundu |
| 3. | Njaa |
| 4. | Wewe mwanamke |
| 5. | Una maana kusema mimi nitaweza kuwauzeni nyinyi nyote pamoja na watu wangu? |
| 6. | Ningalikuwa ntu wa nzungu ningelikuwa hivi |
| 7. | Kuna moshi, naona moshi! Penye moshi pana moto. Karibu kutakuwa na moto |
| 8. | Moto wa mbali hauunguzi |
| 9 | Tuazime mtoto wako |
| 10 | Wanawake wakubwa nyie |
| 11 | Joto |
| 12 | Jua kali |
| 13 | Jua lilitia joto katika miili yetu, joto la huruma katika mioyo yetu |
| 14 | Mmatumbi akipigwa, mzaramo ndiye atapiga kelele za maumivu |
| 15 | Katika daraja hii tutakuwa kitu kimoja |
| 16 | Haya ni maji ya maisha. hii ni silaha yetu. Huu ni usinga ï usinga wa nguvu |
| 17 | Maji haya yatamlainisha samba |
| 18 | Maji haya yataifanya risasi chembe ya mchanga juu ya vifua vyenu |

| | |
|---|---|
| 19 | Hamuko tayari kupigana, muko tayari kupiganiwa. Pepo, maji ndiyo munayotegemea |
| 20 | Usilete taa kalibu. Ondoa muangazaé walisema wataleta muangazaé kutoa giza é lakini nimetambua muangaza wao una hatali zaidi. Afazali kiza hiki. Afazali kiza hiki. Afazali utumwa wa mwili kuliko utumwa wa akili unaoletwa na muangaza |
| 21 | Kwa nini anataka kutuuza sisi watoto wake kwa mabwana wengine |
| 22 | Binadamu huzaa neno |
| 23 | Mpe panga mwananke huyu |
| 24 | Somanga amekuwa kichwa kikubwa |
| 25 | Maji ya maisha |
| 26 | Udongo mwekundu ataondoka. Tutamfagilia mbali pwani |
| 27 | Leo tumepata nguvu mpya. Leo tumepata moyo mpya |
| 28 | Wanaimba maji maji huku wanafyekwa na lisasi |
| 29 | Mala ilianza kutema lisasi |
| 30 | Neno limezaliwa |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Kinjeketile* (2014)

Jedwali namba 4.12, linawasilisha mifano ya sitairi ambazo zimetumika katika tamthiliya ya *Kinjeketile* ambapo Msanii ametumia sitiari ambazo zinalinganisha na kuhusianisha vitu ama dhana zisizohusiana. Kwa mfano tazama katika Jedwali namba 4.12, sitiari na maana zake kama zilivyobainishwa wakati wa majadiliano ya vikundi.

**Jedwali Namba 4.13:Maana za Sitiari**

| Namba | Sitiari | Maana ya ziada |
|---|---|---|
| 1. | Udongo mwekundu | Mzungu (Mjerumani) |
| 2. | Wanawake wakubwa nyie | Wanaume waoga |
| 3. | Maji | Silaha ya ukombozi |
| 4. | Muangaza | Uhuru wa bendera (ukoloni mamboleo) |
| 5. | Kiza | Ukoloni |
| 6. | Njaa | Unyanyaswaji, ukandamizwaji, uonevu, umaskini |
| 7. | Simba | Mkoloni, adui (mjerumani) |

Chanzo: Data za utafiti (2014)

Katika Jedwali namba 4.13 tunaona kuwa sitiari imetumika kuwasilisha dhana tofauti ili kujenga maudhui ya kazi ya fasihi kisitiari. Kwa mfano wanawake limetumika kurejelea wanaume ambao ni waoga wanashindwa kufanya maamuzi, hapa sifa a mwanamke ya uoga inahamishiwa kwa mwanaume.

### 4.6.2 Takriri

Katika kuchunguza na kuchambua tamthiliya ya *Kinjeketile*, utafiti huu ulibaini kuwa msanii ametumia takriri katika kujenga maudhui ya kazi yake, Jedwali namba 4.14 linawasilisha mifano ya takriri iliyotumika katika tamthiliya ya *Kinjeketile.*

Mifano katika Jedwali namba 4.14 inadhihirsha kuwa takriri imetumika kisanii kujenga maudhui ya tamthiliya hii, takriri imetumika kama mbinu ya kuhamasisha harakati za ukombozi, kuhimiza ushujaa kwa mfano katika mfano namba 1 hapo juu, matumizi ya takriri óTokeni! Tokeni, wanawake wakubwa nyi!ô hapa msanii anahimiza ushujaa kwa kuwafananisha wanaume na wanawake huku akitumia takriri óTokeni! Tokeniô.

**Jedwali Namba 4.14:Matumizi ya Takriri katika *Kinjeketile***

| Namba | Takriri |
|---|---|
| 1. | Tokeni! Tokeni, wanawake wakubwa nyi! |
| 2.. | Nyinyi mnalishwa ndiyo...wake zenu wanachukuliwa ï ndiyo. Watoto wenu wanachukuliwa ï ndiyo watu wa ndiyo |
| 3 . | Haludi! haludi |
| 4. | Mbona haludi! Jamani mbona haludi |
| 5. | Nkamate! Anataka kujitosa nkamate!!! |
| 6. | Niache! Niache |
| 7. | Taratibu! taraatibu |
| 8. | Nyamaza! Nyamaza! Haifai hivyo |
| 9. | Joto sanaé ama kweli joto sana, joto hili la ajabu |
| 10. | Haya maji ni silaha yetu. Maji ya maisha, maji haya yatamlainisha simbaé maji haya yataifanya risasi chembe ya mchanga juu ya vifua vyenu. Maji haya yatamtoa mzungu |
| 11. | Maji! Maji! Maji! Maji! |
| 12. | Chukueni na aminini maji ya maisha. Chukueni maji ya nguvu. Chukueni na aminini maji yanayotia ushujaa |
| 13. | Maji! Maji! Maji! Maji! |
| 14. | Tuwashukuru wazee, Tushukuru mizimu. Tumshukuru Hongo |
| 15. | Ua-Ua-Ua-Ua |
| 16. | Udongo mwekundu.ua udongo mwekundu ua udongo mwekundu |
| 17. | Sasa tuko tayari, tuko tayari kwa vita |
| 18. | Vita! Vita! Vita! |
| 19. | Nimetambua, nimetambua kuwa mwangaza wao una hatali |
| 20. | Afazali kiza hiki. Afazali kiza hiki. Afazali utumwa wa mwili kuliko utumwa wa akili unaoletwa na muangaza |
| 21. | Tumekaa, tumekaa tumechoka kungojea |
| 22. | Tuko tayali! Tuko tayali! Tuko tayali! |
| 23. | Tuanze! Tuanze! Tuanze! Tuanze! |
| 24. | Mmechukua nini? Miyanzié ya kufanyia nini? Kuua! Kuua! Kuua! |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Kinjeketile* (2014)

Aidha katika mfano namba 10, msanii ametumia takriri ómajiô kuwapa watu imani na matumaini ya silaha ya harakati za ukombozi mfano anasema óHaya maji ni silaha yetu, maji ya maisha, maji haya yatamlainisha simbaé maji haya yataifanya risasi chembe ya mchanga juu ya vifua vyenuô. Katika mfano namba 15 na 16, msanii anatumia takriri neno óuaô kuhimiza vita dhidi ya mkoloni. Mfano anasema óMaji haya yatamtoa mzungu Udongo mwekundu..ua udongo mwekundu ua udongo mwekundu Chukueni na aminini maji ya maishaô.

### 4.6.3 Tashibiha

Utafiti huu ulichunguza na kubainisha tashibiha zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Kinjeketile* tashibiha imejitokeza kama ifuatavyo katika mifano ifuatayo:

**Jedwali Namba 4.15:Tashibiha katika *Kinjeketile***

| Namba | Tashibiha |
|---|---|
| 1. | Sisi kama wanawake tunantazama tu |
| 2. | Sisi kama wanawake tumekaa tunantazama tu |
| 3. | Nnakuja kama wezi kuja kunisaidia |
| 4. | Afazali kufa kuliko kukaa hivi tunatawaliwa, tunalimishwa kama wanyama |
| 4. | Nimesikia habari ya Bunduki kubwa inayomwaga lisasi kama mchanga |
| 5. | Mutagombana wenyewe kwa wenyewe, kabila na kabila kama paka na mbwa |
| 6. | Na kama mibaazi tutatambaa |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Kinjeketile* (2013)

Jedwali namba 4.15 linaonyesha baadhi ya tashibiha zilizojitokeza katika tamthiliya ya Kinjeketile, kwa mfano, katika mfano namba 1 msanii anasema ósisi kama wanamke tunatazama tuô hapa msanii analinganisha wanaume na wanawake. Dhana hii inatumika kuonyesha udhaifu wa wanaume kutokuchukua hatua za kijasiri kupambana na unyonyaji unaofanywa na Wajerumani. Kitendo hiki kinalinganishwa na wanawake amabao jamii huwatazama kama viumbe waoga na wasio jasiri wasioweza kufanya maamuzi magumu.

### 4.6.4 Tashihisi

Tamathali hii ilionekana kutumiwa sana na msanii katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*. Mfano ifuatao katika Jedwali namba 4.16 inadhihirisha ujitokezaji wa tamathali hii.

**Jedwali Namba 4.16:Mfano ya Tashihisi katika *Kinjeketile***

| Namba | Tashihisi |
|---|---|
| 1. | Mapenzi haya yatatuunganisha tutakuwa kitu kimoja |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Kinjeketile* (2013)

Jedwali namba 4.16 linaonyesha tashihisi zilizojitokeza katika kinjeketile, ukichunguza mifano hiyo utaona kuwa tashihisi hutumika kwa kuvipa vitu visivyo na uhai uhai na uwezo wa kutenda kama binadamu (rejea pia Kahigi na Mugyabuso, 1979; Cuddon, 1998; Alembi, 2000).

## 4.7 Dhima ya Vipengele vya Lugha katika *Morani* na *Kinjeketile*

Utafiti huu ulichunguza dhima ya vipengele vya lugha katika tamthiliya ya *Kinjeketile* na *Morani*. Ili kufikia lengo hilo, utafiti huu ulibainisha vipengele vya

lugha ambavyo vinajitokeza katika tamthiliya hizo na kisha wakati wa majadiliano ya vikundi mtafiti aliweza kuwahoji wahojiwa ili kubaini vipengele vya lugha vilivyotumikia katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile* vina dhima gani? Matokeo yalikuwa kama yanavyojibainisha katika sehemu zifuatazo:

### 4.7.1 Kuwasilisha Dhamira Kuu za Tamthiliya

Wakati wa majadiliano ya vikundi wahojiwa walieleza kuwa vipengele vya lugha kama vile sitiari, tashibiha, takriri methali vimetunmika katika kujenga maudhui ya kazi hizo za fasihi. Kwa mfano katika kuwasilisha suala la ujenzi wa jamii mpya, msanii wa *Morani* ametumia sitiari mbalimbali tazama jedwali lifuatalo.

**Jedwali Namba 4.17:Dhamira katika Sitiari (*Morani*)**

| Namba | Sitiari | Dhamira |
|---|---|---|
| 1. | Huu ni wakati wa kunoa mashoka | Kupamabana, vita |
| 2. | Nguzo ya uswezi | Ukombozi |
| 3. | Bundi | Maadui |
| 4. | Kivuli | Unafiki |
| 5. | Kama wewe umenunuliwa siyo mimi | Kupewa rushwa |
| 6. | Hatuwezi kuwaacha mapapa tukavua pelege | Matajiri (mapapa) na maskini (pelege) |

**Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Morani*, Juni, 2014**

Katika jedwali namba 4.17 hapo juu linawasilisha mifano ya sitiari na dhamira inazowawasilisha kama ilivyotumika katika tamthiliya ya *Morani*. Dhima ya sitiari katika *Morani* haina tofauti na dhima ya sitiari katika tamthiliya ya *Kinjeketile* ambapo wahojiwa walibaini dhima za matumizi ya sitiari katika tamthiliya *Kenjeketile* kama inavyojionesha katika jedwali.

**Jedwali Namba 4.18:Dhamira katika Sitiari *Kinjeketile***

| Na. | Sitiari | Dhamira |
|---|---|---|
| 1. | Udongo mwekundu | Mkoloni (Mjerumani) |
| 2. | Njaa | Umaskini |
| 3. | Una maana kusema mimi nitaweza kuwauzeni nyinyi nyote pamoja na watu wangu? | Kupokea rushwa na usariti |
| 4. | Wanawake wakubwa nyie | Waoga |
| 5. | Mmatumbi akipigwa, mazaramo ndiye atapiga kelele za maumivu | Umoja |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Kinjeketile* (2014)

Jedwali namba 4.18 linawasilisha mifano ya sitiari na dhamira inayowasilisha kama ilivyotumika katika tamthiliya ya *kenjeketile.* Katika mifano hiyo tunaona kuwa sitiari imetumika kuwasilisha harakati za ukombozi na vikwazo vinavyoikumba harakati hizo, msanii anatumia sitiari udongo mwekundu kurejelea mzungu ama Mjerumani ambaye ndiye mkoloni. Sitiari hii ina dhima ya kuonyesha udhalimu wa wakoloni kwa jamii. Aidha kwa kutumia sitiari ónjaaô msanii anarejelea suala la umaskini katika jamii. Dhima ya sitiari hii ni kuonyesha jinsi ukoloni ulivyosababisha umaskini kwa jamii. Kwa upande mwingine msanii ametumia sitiari kuwasilisha suala la umoja, uoga, rushwa na usaliti katika jamii.

Utafiti huu ulibaini kuwa, vipengele vyua lugha vilivyotumika katika tamthiliya za *Morani* na *Kinjeketile* zina dhima ya kuwasilisha maudhui ya kifasihi, kubainisha uovu ndani ya jamii, kueleimisha, kukosoa na kuiamsha jamii. Vipengele vya lugha vimetumika kubeba na kujenga maudhui ya kazi hizo za fasihi kwa kubaini harakati za ukombozi, ujenzo wa jamii mpya, mapinduzi, vita dhidi ya dhuluma, rushwa, nafasi ya mwanamke, imani ya jadi, usaliti na uongozi mbaya. Kwa mfano katika

kuliwasilisha suala la usaliti msanii wa *Morani* anasema tamthiliya zote mbili zimezungumzia juu ya usaliti katika harakati za mapinduzi na ukombozi wa jamii.

Kwa mfano katika tamthiliya ya *Morani* msanii anasema ôWachawi ndiyo, wachawi hawa hutembea uchi wa mnyama, wakati wa usiku wa manane, wakati blanketi la njozi za matumaini na njaa limewafunika wafanyakazi na wakulima waliopondeka nguvu za mishipa yao kwa kumiminiwa jasho lao ili kuyanenepesha mashavu ya wachawi hawaô kwa kutumia sitiari msanii anawasilisha juu ya suala la usaliti, kwa mfano katika kuwasilisha suala la rushwa msanii kwa kumtumia mhusika Jalia anasema ôkama wewe umenunuliwa sio mimiô kwa kutumia neno ôkununuliwa msanii anarejelea kupewa rushwa kwa Mlemeta na Yusufu ili kuharibu zoezi la kuwabaini wahujumu uchumi.

Katika *Kinjeketile* uk.5 anasema ôHili haliwezi kufanyika mara moja, tena basi itakuwa vigumu kulifanya maana hivi sasa kuna vibalaka chungu nzima. ôUtakachofanya akina askari au mnyampala kashasikia, tumeshikwa na njaa na njaa hii intaufanya tuuzane, kwa hiyo kuyapeleka mambo haya mbio mbio haifai, tuna maadui na katika sisi wenyewe kuna maaduiô. Hapa msanii anatumia neno ônjaaô kurejelea umaskini ambao unasabasha watu kula rushwa na kuwasaliti wenzao katika kuwasilisha usaliti anatumia sitiari ôtuuzaneô kurejelea usaliti.

### 4.7.2 Kulinganishi na Kulinganisha Uteuzi wa Vipengele vya Lugha na Suala la Kihistoria

Utafitri huu ulichambua na kuchunguza vipengele vya lugha vilivyotumika katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile* ili kuona ni jinsi gani wasanii wa tamthiliya hizo

wanatumia vipengele vya lugha katika kuwasilisha suala la kihistoria. Je, kuna kufanana ama kutofautiana katika uteuzi wa vipengele vya lugha ili kuwasilisha masuala ya kihistoria katika jamii? Matokeo ya utafiti huu yalikuwa kama yanavyowasilishwa katika vipengele vifuatavyoò.

### 4.7.3 Kutofautiana

Katika uchunguzi wetu, utafiti huu ulibaini kuwa, wasanii wametumia vipengele vya lugha kwa namna tofauti na uteuzi wa viepengele huo unatofautiana kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano ilibainika kuwa katika *Morani* msanii ametumia zaidi sitiari pana kuwasilisha suala la ujenzi wa jamii mpya kama moja ya historia ya nchi ya Tanzania katika kipindi cha wahujumu uchumi na harakati za kuwafichua na kuwakamata. Hivyo *Morani* inahusu harakati za ukombozi kutoka katika utawala wa ukoloni mamboleo ambapo wanyonge wananyonywa na kundi la watu wachache ambao ni Waafrika wenzao. Tofauti na *Kinjeketile* ambayo inawasilisha suala la kihistoria hasa katika harakati za ukombozi kutoka katika ukoloni mkongwe, ukoloni chini ya Mjerumani.

Utafiti huu ulibaini kuwa *Kinjeketile* inatumia sitiari óudongo mwekunduô kurejelea wakoloni ama Mjerumani wakati katika *Morani* msanii anatumia sitiari ómapapaô kuwasilisha wakoloni wazawa ambao wananyonya na kuhujumu uchumi wa nchi wakati umma ukihangaika na umaskini. Silaha ya vita vya ukombozi inayotumika katika *Kinjeketile* ni suala la uhalisia ambalo lilitumiwa na wapiganaji wa kusini dhidi ya Mjerumani. Msanii anatumia dhana ya ómajiô kuwasilisha uhalisia na jinsi watu walivyouwawa na Mjerumani kwa imani ya msaada wa mizimu ambayo inasadikiwa kuwapa maji kama silaha yao dhidi ya Mjerumani.

Hivyo tunaona kuwa tamthiliya hii imetumia lugha ya kawaida zaidi katika kuwasilisha suala la wa harakati za ukombozi katika jamii. Historia inamwonyesha *Kinjeketile* ambaye aliwaaminisha watu wa kusini kuwa maji yanaweza kupambana na silaha ya bunduki aliyokuwa akitumia mkoloni. Hatimaye watu walimwamini na kuingia vitani. Jambo hili pia linaelezewa na Ebrahim Hussein katika tamthiliya ya *Kinjeketile.* Wakati wa usaili na majadiliano ya vikundi wahojiwa walieleza kuwa msanii ametumia sanaa kuwasilisha historia katika uhalisia wake, hata lugha aliyotumia ni ya kawaida ambayo inawafanya wasomaji waone kama msanii alikuwa anaandika historia ya vita vya watu wa kusini dhidi ya Mjerumani kwa kutumia mchezo wa kuigiza, pia ilielezwa kuwa tamthiliya hii haijafumwa kisanii bali ipo wazi.

Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa tamthiliya hizi zinatofautiana katika kutumia ufundi wa kisanii katika uteuzi na matumizi ya lugha kibunifu katika kuwasilisha dhamira mbalimbali. Kwa mfano, wahojiwa walibainisha kuwa, *Morani* imetumia lugha ya picha, taswira na jazanda mbalimbali na hatimaye kujenga sitiari pana ambayo imetumika kama mbinu ya kuwasilisha maudhui ya kazi yake. Kwa mfano matumizi ya; óDongoô, óBundiô, óMkuyuô hayo yakiwa baadhi ya maneno amabyo yametumika kama sitiari kujenga maudhui ya tamthiliya ya *Morani*.

Ukichunguza mifano hiyo, utaona kuwa, msanii ametumia lugha ya picha na taswira mbalimbali kujenga maudhui ya kazi yake. Ubunifu huu ni tofauti na tamthiliya ya *Kinjeketile* ambaye ametumia lugha ya mazungumzo ya kawaida amabyo hayampi nafasi msomaji kufikiri dhamira ya mwandishi kwa mfano katika uk. 5 anasema ówewe mwanamke Wamatumbi waogaô, ósisi sote tunataka Mjerumani aondokeô

lugha iliyotumika katika mifano hiyo ipo wazi na msomaji anaweza kuitafsiri bila shida. Tofauti na *Morani* ambayo inamfanya msomaji atafsiri dhamira ya mtunzi katika matumizi ya sitiari, taswira na picha alizotumia kujenga dhamira hizo.

Tofauti nyingine ni suala la kihistoria ambalo tamthiliya hizi zinawasilisha; *Morani* inatumia mbinu zafasihi simulizi inayomfanya msanii kuandika kazi yake kama anasimulia hadithi japo ni kazi ya kitamthiliya ambapo anawasilisha suala la kihistoria la jamii ya Tanzania huru katika harakati za ujenzi wa jamii mpya yenye usawa na umiliki sawa wa mali. Jamii isiyokuwa na matabaka na kuundoa ukoloni mkongwe, Mfano msanii anamtumia mwanamke Jalia kuongoza mapambano dhidi ya wahujumu uchumi, msanii anasema óilikaona mizuka inalima shamba la tajiri wao na ilikuwa siku, watu wote pale kijijini walikuwa wamelala lakini mizuka hii iliyokongoroka mifupa, nywele zilizotimka, ngozi zao kama gamba la mbuyu ilipanda migongo yao na kuendelea kulima, bila kupumzika wala kupumuaé enyi viumbe kwa nini mwateseka hivyo?

Kwa nini mwatumikishwa hivyo? Hamwoni kuwa mwadhulumiwa... ilikuwa kazi bure ile mizuka haikujibu kitu kwani ndimi zao zilikuwa zimekatwa na bwana waoé dongo halikulidhika lazima niwafumbue machoé juhudi zake hazikufika mbali, kwani bwana mizuka aligundua siri hii akalikamata lile dongo akalifinyanga, akalichanganya na udongo likawa mbolea ya shamba lake. Na mizuka ikazidi kusotaô kwa kutumia maneno hayo tunaona kuwa msanii anatumia sitiari na taswira kuwasilisha suala la ukandamizaji, unyonyaji, utumikishwaji, umaskini na harakati za ukombozi. Msanii anaonyesha jinsi mkoloni mambo leo ulivyowageuza wananchi wasione wanachofanyiwa na wasiweze kusema wala kujikomboa.

Hata Yule aliyetaka kuwakomboa ukoloni mambo leo ulihakikisha unammaliza na kumziaba mdomo. Tofauti na *Kinjeketile* ambayo inatumia lugha rahisi na ya kawaida kuwasilisha suala la harakati za ukombozi kutokana na ukoloni mambo leo. Inahusu jamii inayotawaliwa na wakoloni na wakoloni. Kwa mfano uk. 1 msanii anamtumia BI KITUNDA anasema ósiwe njaa namna gani, wanaume wenyewe wote wanalima shambani kwa Bwana Kinoo? Njaa itakosa?  kwa maneno hayo msanii anaonyesha jinsi jamii ilivyokuwa maskini kwa kutumikishwa katika mashamba ya mabwana zao wakati familia zao zikifa kwa njaa. Aidha msanii anaonyesha jinsi ukandamizaji na uzalilishaji ulivyokuwa kwa kupigwa viboko na kutumikishwa mfano uk. 3 anasema óKitunda aliinuka kunyosha mgongo, mnyapala akampiga viboko, Kitunda hakukubali alikikamata kiboko. Pale pale jumbe akaja akaamrisha akamatwe atandikweô. Hapa msanii anaonyesha unyanyasaji wa jamii uliokuwa ukifanywa na mkoloni na vibaraka wake.

Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa zipo mbinu za kimtindo ambazo zinazitofautisha tamthiliya hizi. Mbinu hizo ni kama zinavyojizihirisha katika jedwali namba 4.22 hapa chini.

**Jedwali Namba 4.19: Mbinu za Kimtindo Zinazotofautisha *Morani na Kenjeketile***

| **Namba** | ***Mbinu ya kimtindo*** | ***Kenjeketile*** | **Morani** |
|---|---|---|---|
| 1. | Mbinu ya kiishara | Haijatumika | Imetumika |
| 2. | Mbinu ya kisitiari | Haijatumika | Imetumika |
| 3. | Mbinu ya Korasi | Haijatumika | Imetumika |
| 4. | Mbinu ya kejeli | Haijatumika | Imetumika |
| 5. | Motifu ya Safari | Haijatumika | Imetumika |
| 6. | Mbinu ya majigambo | Haijatumika | Imetumika |

Chanzo: Data za utafiti (2013)

Jedwali namba 4.19 linadhihirisha mbinu za kimtindo ambazo zinatofautisha tamthiliya ya *Kinjeketile* na *Morani*, ilibainika kuwa tamthiliya ya *Morani* imetumia mbinu za kisanii zaidi katika kuwasilisha suala la kihistoria. Mbinu zilizotumika za kisitiari, korasi, majigambona motifu ya safari zinaifanya tamthiliya ya *Morani* ionekane kuwa ni yenye ófumboô ama kitendawili kinachotakiwa msomaji atumie mbinu za uhakiki wa kifasihi katika kukitegua.

Hili linajidhihirisha katika onyesho la kwanza la tamthiliya ya *Morani,* ambapo msanii anatumia motifu ya safari katika kuusaka ukweli, kwa kuwatumia wahusika Mzee, Malongo na Mapoto. Aidha, msanii anatumia mbinu ya majigambo kwa mfano Nungunungu anatamba kuwa wao ndiyo walioifanya nchi iwe kama ilivyo. Tofauti na tamthiliya ya *Kinjeketile* ambayo ipo wazi na haihitaji kufikiri ili kubaini alichokusudia mtunzi.

Japo kuwa ilielezwa katika majadiliano ya vikundi kuwa mbinu za kimtindo zilizotumika zilitofautiana katika kiwango cha utumizi na kubainisha upekee wa mtunzi kutoka na ufundi alionao wa utungaji wa kazi ya kifasihi. Kwa ujumla tamthiliya ya *Morani* ni tamthiliya ya majaribio ambayo imetumia zaidi mbinu za fasihi simulizi ya Kiafrika katika kuwasilisha maudhui yake.

Kwa mfano matumizi ya wimbo, majigambo, wahusika wasio watu kama vile dongo wahusika wa kufikirika. Utafiti huu unaichukulia *Kinjeketile* kama tamthiliya iliyojikita katika utunzi wa Kiaristotle kwa sababu inazungumzia juu ya mhusika aliyeaminiwa na watu na hatimaye kuanguka. Vile vile, ni tamthiliya ambayo imejikita zaidi katika majibizano ya wahusika.

### 4.7.4 Kufanana

Utafiti huu uligundua kuwa, tamthiliya ya *Kinjeketile* na *Morani* zinatofautiana zaidi kuliko kufanana. Kufanana kwa tamthiliya hizi kunatokana na sababu kwamba zote zinawasilisha masuala ya kihistoria japo kwa mbinu tofauti za kisanaa na pia vipindi tofauti vya kihistoria. Hivyo basi, ni vigumu sana kutoa hitimisho kuwa tamthiliya hizi zinafanana. Katika usaili walimu na wanafunzi wa fasihi Chuo Kikuu wanasema kuwa tamthiliya hizi zinafanana katika uteuzi na matumizi ya tamathali za semi, tazama katika Jedwali Namba 4.20.

**Jedwali Namba 4.20:Kufanana katika Uteuzi wa Tamathali za Usemi**

| Namba | *Morani* | *Kenjeketile* | Kufanana |
|---|---|---|---|
| 1. | Sitiari | Sitairi | ã |
| 2. | Tashibiha | Tashibiha | ã |
| 3. | Tashihisi | Tashihisi | ã |
| 4. | Takriri | Takriri | ã |

**Chanzo: Data za utafiti (2014)**

Jedwali namba 4.20 linadhihirisha kuwa tamthiliya ya *Morani* na *Kenjeketile* zinafanana katika matumizi ya tamathali za usemi kama inavyojidhihirisha katika jedwali hilo.

Utafiti huu uligundua kuwa tamthiliya hizo zinafanana katika kuwasilisha dhamira mbalimbali kwa kutumia vipengele vya lugha. Sehemu ifuatayo inajadili vipengele vya lugha na dhamira zinazowasilishwa.

## 4.8 Dhamira za *Morani* na *Kenjeketile*

Katika usaili na wanafunzi wa fasihi Chuo Kikuu ilielezwa kuwa Mwandishi E. Hussein na Emmanuel Mbogo wanafanana katika utunzi wa tamthiliya kwa sababu wote wawili wamejikita kujadili juu ya masuala ya kihistoria.

**Jedwali Namba 4.21:Kufanana kwa Dhamira Zinazowasilishwa na Vipengele vya Lugha**

| Namba | Dhamira katika *Morani* | Dhamira katika *Kenjeketile* |
|---|---|---|
| 1. | Unyonyaji na ukandamizaji | Unyonyaji na ukandamizaji |
| 2. | Hali ngumu ya uchumi | Hali ngumu ya uchumi |
| 5. | Mapinduzi na harakati za Ukombozi | Mapinduzi na harakati za ukombozi |
| 6. | Rushwa | Rushwa |
| 7. | Matabaka | Matabaka |
| 8. | Nafasi ya mwanamke | Nafasi ya mwanamke |
| 9. | Uongozi mbaya na Matumizi mabaya ya madaraka | Uongozi mbaya na Matumizi mabaya ya madaraka |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika *Morani* na *Kenjeketile* (2013)

Kielelezo hicho namba 4.21 kinaonesha dhamira ambazo zinajitokeza katika tamthiliya zote mbili, ambapo ni kupitia vipengele vya lugha katika mtindo dhamira hizo huwasilishwa ambapo kwa kutumia vipengele hivyo dhamira zinazofanana katika tamthiliya hizo zimejitokeza.

### 4.8.1 Matabaka

Waandishi wote wanafanana katika uibuaji wa matabaka ambapo wote wanaonesha matabaka yaliyopo katika jamii. Tabaka la watawala na tabaka la watawaliwa. Mfano katika *Kenjeketile* matabaka yanajitokeza baina ya tabaka la wakoloni na wananchi. Katika *Morani* kuna tabaka la walionacho na wasionacho msanii anasema ómapapaô na ópelegeô.

### 4.8.2 Nafasi ya Mwanamke

Tamthiliya zote mbili zinabainisha nafasi ya mwanamke japo utafiti huu ulibaini kuwa nafasi ya mwanamke katika tamthiliya hizo inatofautiana, katika tamthiliya ya

*Morani* mwanamke amechorwa kama shujaa, jasiri na mpigania haki na mwanamapinduzi. Tofauti na tamthiliya ya *Kinjeketile* ambapo mwanamke amechorwa kama kiumbe tegemezi anayetegemea nguvu za mwanaume.

### 4.8.3 Uongozi Mbaya

Waandishi wa tamthiliya zote mbili wanazungumzia juu ya uongozi mbaya katika jamii. Mfano katika *Kenjeketile*, mwandishi anamtumia *Kinjeketile* kama kiongozi anayekwepa majukumu yake baada ya kuwaletea watu maji anashindwa kutoa ruhusa ya kuanzisha vita dhidi ya Mjerumani. Wakati katika *Morani* uongozi mbaya unajitokeza kwa viongozi ambao wamepewa mamlaka katika jamii lakini wanashindwa kuyatekeleza kwa haki na usawa zaidi ya kuwa wasaliti na wala rushwa mfano ni Mlemeta na Yusufu.

### 4.8.4 Rushwa na Usaliti

Suala la rushwa limezungumziwa katika *Kenjeketile* ambapo msanii anaongelea juu ya rushwa na usaliti ambapo wapigania uhuru wanakuwa wasaliti na kutoa siri za harakati za mapinduzi kwa watawala kama vile manamba na mnyampala. Aidha, katika *Morani* mtunzi anaonyesha rushwa na usaliti ambapo Yusufu na Mlemeta wanapokea rushwa kutoka kwa Nungunungu na hatimaye kusaliti harakati na zoezi zima la kuwakamata wahujumu uchumi.

Kwa mfano katika *Morani* kwa kumtumia mhusika Jalia msanii anasema ôkatikati hakuna wahujumu, ôWahujumu wako juu, hatuwezi kuwaacha mapapa tukavua pelegeö. Aidha, msanii anasisitiza kwa kumtumia Dongo msanii anasema ôMlemeta katika mapambano haya msumeno utakata pande zote. Aidha tufanye kazi ama

tuache, lakini hatuwezi kuchanganya kazi na unafiki, kama tumekubaliana kwa pamoja kuwa wahujumu wote wakamatwe, basi watakamatwaö

### 4.8.5 Mapinduzi na Harakati za Ukombozi

Suala la mapinduzi ni suala ambalo limejitokeza katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile.* Katika *Morani* mwandishi anaonyehsa harakati za mapinduzi na ukombozi wa jamii kutoka katika ukoloni mamboleo wakati katika *Kinjeketile* mwandishi anaonyesha harakati za mapunduzi na ukombozi kutoka katika ukoloni mkongwe wa Mjerumani.

### 4.8.6 Unyonyaji na Ukandamizaji

Wasanii wote katika tamthiliya hizi wamezungumzia suala la unyonyaji na ukandamizaji ambalo linafanywa na watawala. Katika *Morani,* mtunzi anaongelea unyonyaji unaofanywa na Nungunungu na wenzake ambao wanajilimbikizia mali na kuuacha umma ukiwa maskini. Kwa upande wake *Kinjeketile* anaongelea unyonyaji na ukandamizaji unaonfanywa na mkoloni Mjerumani amabpo wananchi na nguvu kazi inaelekezwa katika mashamba ya mkoloni huku jamii ikifa kwa njaa na umaskini wa kukosa chakula.

### 4.8.7 Hali Ngumu ya Uchumi

Tamthiliya zote zimejadili juu ya hali ngumu ya uchumi inayosababishwa na uongozi na utawala wa wakoloni. Katika *Kinjeketile* hali ngumu ya uchumi inasababishwa na utawala wa Mjerumani wakati katika *Morani* hali ngumu ya uchumi inasababishwa na ukoloni mamboleo ambapo baadhi ya wananchi wachache wanajilimbikizia mali wakati wengi wanakufa kwa umaskini uliokithiri. Kwa mfano

katika *Kinjeketile* mwandishi anasema óBI KITUNDA; Bule tu. Hata huyo mume wangu akiludi sina cha kumpa. Nimetafuta walau muhogo, hata sikupata; na mizizi inatisha. Ntoto wa Bi Bobali amekufa kwa hiyo hiyo mizizié .

Basi tulipoona moshi tukafikiri unapika, maneno haya yanadhihirisha umaskini ambao umekithiri katika jamii. Katika *Morani* msanii anasema ókwanza tazama. Juhudi yote tuliyofanya katika ile safari imekuwa kazi bure. Safari ilikuwa ndefu; usiku, mchana, mvua, miba, njaa, kiué lakini matokeo yake ni haya. Akina Nungu wanatumbua, akina yakhe wanazidi kutumbukiaô hapa msanii anaonyesha jinsi baadhi ya wachache wanavyonufaika na matunda ya uhuru amabo wananchi waliupigania kwa nguvu na jasho lao.

### 4.8.8 Hitimisho

Sura hii imewasilisha na kujadili data na matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu kulingana na malengo mahususi ya utafiti kama yalivyobainishwa katika sura ya kwanza. Sura hii imebainisha vipengele vya lugha ambavyo vimetumika katika tamthiliya zilizochunguzwa katika utafiti huu ambazo ni *Morani* na *Kinjeketile.*

Utafiti huu umebaini kuwa tamthiliya ya *Morani* imetumia vipengele vya lugha kama vie tamathali za usemi na methali. Imejadiliwa katika suara hii kuwa *Morani* imetumia lugha ya kitamathali zaidi katika kuwasilisha maudhui ya kazi yake na hivyo kumfanya msomaji aweze kufikiri zaidi ili kuweza kubaini kile msanii alichokusudia. Wakati *Kinjeketile* imetumia lugha ya kawaida na iliyo wazi zaidi ambayo haimtaki msomaji kufikiri ili kuweza kubaini kile anachokiwasilisha msanii. Imejadiliwa kuwa vipengele vya lugha vilivyotumika katika tamthiliya teule

vimelenga kuwasilisha dhamira kuu za tamthiliya hizo kama vile ujenzi wa jamii mpya, harakati za ukombozi na mapinduzi, hali ngumu ya uchumi, nafasi ya mwanamke, unyonyaji na ukandamizaji, rushwa na usaliti. Suala hii imejadili kuwa, tamthiliya hizi zinatofutiana katika kuwasilisha suala la kihistoria kwa sababu wasanii wanawasilisha historia ya jamii ya Tanzania katika vipindi viwili tofauti. *Morani* anawasilisha historia katika kipindi cha baada ya uhuru na hivyo kujadili juu ya historia ya harakati za kupambana na ukoloni mamboleo wakati *Kinjeketile* inajadili kwa uhalisia juu ya harakati za jamii za kusini katika kupambana na ukoloni wa Mjerumani, yaani, ukoloni katika utawala wa Mjerumani na imani ya maji yanayoweza kuibadili risasi kuwa maji.

Kwa upande mwingine ilibainika kuwa tamthiliya hizi kwa vile zimendikwa na wasanii wa jamii moja ambao wameshuhudia na kupata masimulizi ya historia ya jamii yao. Wasanii hawa wanafanana katika kuwasilisha maudhui ya kazi zao ambapo wote kwa pamoja wanajadili juu ya mambo mbalimbali yaliyopo katika jamii kama vile; rushwa, harakati za ukombozi, usaliti, unyonyaji na ukandamizaji. Aidha, sura hii imebainisha na kujadili dhima za vipengele vya lugha katika tamthiliya teule.

# SURA YA TANO

# 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho ambayo inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni; sehemu ya kwanza inahusu muhtasari, sehemu ya pili inahusu hitimisho la utafiti huu na sehemu ya tatu ni mapendekezo ya utafiti huu.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ni utafiti linganishi ambao ulilenga kulinganisha dhima ya mtindo katika tamthiliya za Kihistoria kwa kulinganisha tamthiliya ya *Morani* iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo na tamthiliya ya *Kinjekeitile* iliyoandikwa na Ebrahim Hussein. Lengo ni kutaka kuibua vipengele vya lugha ambavyo vimetumika katika kuwasilisha suala la kihistoria katika jamii na kuvilinganisha kutoka kwa msanii mmoja na msanii mwingine.

Tatizo la utafiti huu ni kutaka kuchunguza dhima ya vipengele vya kimtindo katika tamthiliya za kihistoria kwa kulinganisha tamthiliya za *Morani* na *Kinjeketile* ili kuona ni jinsi gani wasanii wa tamthiliya hizo wanafanana ama kutofautiana katika uteuzi wa vipengele vya kimtindo wanapowasilisha suala la kihistoria. Aidha, lengo la utafiti huu kama lilivyobainishwa katika sura ya kwanza ilikuwa ni kuchunguza dhima ya vipengele vya kimtindo katika tamthiliya za kihistoria kwa kulinganisha tamthiliya za *Morani* na *Kinjeketile* ili kubaini vipengele vinavyowafananisha na kuwatofautisha wasanii wa vitabu hivyo katika kuliwasilisha suala la kihistoria.

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi matatu ambayo ni; Kubainisha vipengele vya lugha katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile*; kubaini dhima ya vipengele vya lugha vilivyobainishwa na kulinganisha na kulinganua uteuzi wa vipengele vya kimtindo katika kuwasilisha suala la Kihistoria.

Ili kufikia malengo hayo, utafiti huu ulikusudia kujibu maswali matatu ambayo ni; Je, ni vipengele vipi vya lugha vinavyojitokeza katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile*? Je,vipengele vya lugha vilivyobainishwa katika namba (i) hapo juu vina dhima gani? Je, uteuzi wa vipengele vya lugha katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjekitile* vinafanana ama kutofautiana katika kuwasilisha suala la Kihistoria?

Pamoja na kuwa kuna tafiti ambazo zimefanywa kuhusu ulinganishaji wa kazi za tamthiliya, lakini ulinganishaji huo haukuzingatia masula ya kihistoria. Vile vile tafiti nyingi zimejikita katika kulinganisha fani na maudhui ya kazi za faishi. Hivyo, bado inaonesha kuwa utafiti wa kina unahitajika ili kutafiti jinsi vipengele vya lugha vinavyoweza kumtofautisha msanii mmoja na msanii mwingine, pengo hili ndilo ambalo utafiti huu umekusudia kuliziba. Ili kufikia lengo na kuziba pengo hilo, utafiti huu basi, umechunguza dhima za Kimtindo katika tamthiliya za kihistoria kwa kutumia mifano ya *Morani* na *Kinjekitile.*

Aidha kulingana na malengo ya utafiti huu, utafiti huu ulitumia nadharia ya elimumitindo ambayo ilionekana inafaa na imetuongoza katika kuchunguza na kuchambua data za utafiti huu. Walengwa waliohusishwa katika utafiti huu ni walimu wa fasihi (Sekondari ya St. Anthon na Chuo Kikuu cha Dar es salaam) na wanafunzi wa fasihi (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na shule ya Sekondari ya St.

Anthon) iliyopo Mbagala Dar es salaam. Vile vile kundi lingine ni watunzi wa tamthiliya zilizotumiwa katika kazi hii na wa karibu wa watunzi. Sampuli ya utafiti huu itateuliwa kwa kutumia mbinu mbili yaani: mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu na uteuzi rahisi wa sampuli.

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu nne ambazo ni; maktaba, usaili, dodoso na majadiliano ya vikundi. Mbinu ya usomaji wa machapisho ilikuwa ni mbinu kuu ambayo ilimsaidia mtafiti kuchambua vitabu vyote viwili na kubainisha vipengele vya kimtindo vinavyotumika kujenga maudhui ya kazi ya sanaa. Aidha mbinu ya dodoso na usaili zilitumika kama mbinu jazilizi ambazo ziliziba mapengo ambayo hayakuwa yameeleweka katika mbinu kuu ya usomaji wa machapisho. Utafiti huu unatumia sifa za utafiti wa kitakwimu na usiokitakwimu. Aidha, data ya utafiti huu imechambuliwa kwa kutumia mbinu mbili, yaani uchambuzi maudhui na uchambuzi linganishi.

Katika kujibu maswali ya utafiti huu, kwa kuanza na swali la kwanza, utafiti huu ulichunguza vipengele vya lugha katika tamthiliya ya *Morani* na kubaini kuwa, msanii ametumia vipengele vya lugha kama vile tamathali za semi na methali. Utafiti huu umegundua kuwa, msanii ametumia sitiari mara nyingi zaidi kuliko tamathali zingine za semi. Aidha utafiti huu umebaini kuwa, *tamthiliya* ya *Morani* ni tamthiliya ya kisitiari inayotumia lugha ya kitamathali katika kujenga maudhui ya kazi yake.

Aidha, vile vile ilibainika kuwa tamthiliya hii ni ya majaribio kwa sababu imefuata misingi ya utaunzi wa tamthiliya unaoingiza vipengele vya fasihi simulizi ya

Kiafrika kama vile nyimbo, hadithi, wahusika wanyama na wasio watu, nyimbo na utanzu ndani ya utanzu mwingine. Aidha, kwa upande mwingine wa tamthiliya ya *Kinjeketile,* utafiti huu umebaini kuwa msanii ameteua vipengele vya lugha kama vile tamathali za semi na methali moja tu.

Utafiti huu ulibaini kuwa tamthiliya ya *Kinjeketile* imejengwa kwa kutumia lugha ya kawaida. Mazungumzo ya wahusika yanatumia lugha ya kawaida ambayo ipo wazi, rahisi na inayoeleweka kwa msomaji. Tamathali za semi zilizotumika ni kama vile sitiari, tashibiha, takriri na tashihisi. Aidha utafiti huu uligundua kuwa tamthiliya ya *Kinjeketile* inawasilisha uhalisia wa historia ya kweli. Hivyo, mtunzi hajatumia lugha ya kisanii katika kuwasilisha suala la historia ya tukio la kweli ambalo lilitokea kwa jamii ya kusini kwa wakati wa vita vya kuupinga utawala wa Mjerumani.

Katika kujibu swali la pili la utafiti huu ambalo lililenga kubainisha dhima ya vipengele vya lugha katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile*. Utafiti huu ulibaini kuwa; vipengele vya lugha vilivyotumika katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile* vina dhima ya kuwasilisha maudhui ya kifasihi, kubainisha uovu ndani ya jamii, kuelimisha, kukosoa na kuiamsha jamii. Vipengele vya lugha vimetumika kubeba na kujenga maudhui ya kazi hizo za fasihi kwa kubaini harakati za ukombozi, ujenzi wa jamii mpya, mapinduzi, vita dhidi ya dhuluma, rushwa, nafasi ya mwanamke, imani ya jadi, usaliti na uongozi mbaya.

Utafiti huu ulibaini kuwa wasanii wa tamthiliya hizi wametumia vipengele vya lugha kwa lengo la kujenga dhamira za kazi zao. Dhamira za tamthiliya hizi zinajidhihirisha katika vipengele vya lugha kama vile sitiari, tashibiha, takriri na

tashihisi. Ingawa uteuzi na utumizi wa vipengele hivyo unatofautiana kutoka tamthiliya moja na tamthiliya nyingine.

Swali la tatu la utafiti huu liliweza kujibiwa kwa data zilizopatikana katika utafiti huu kama ifuatavyo. Katika kulinganisha na kulinganua jinsi wasanii wa tamthiliya za *Morani* na *Kinjeketile* wametumia vipengele vya lugha katika kuwasilisha suala la kihistoria. Utafiti huu ulibaini kuwa; wasanii wametumia vipengele vya lugha kwa namna tofauti na uteuzi wa viepengele huo unatofautiana kwa kiwango kikubwa.

Kwa mfano ilibainika kuwa katika *Morani* msanii ametumia zaidi sitiari pana kuwasilisha suala la ujenzi wa jamii mpya kama moja ya historia ya nchi ya Tanzania katika kipindi cha wahujumu uchumi na harakati za kuwafichua na kuwakamata. Hivyo *Morani* inahusu harakati za ukombozi kutoka katika utawala wa ukoloni mamboleo ambapo wanyonge wanayonywa na kundi la watu wachache ambao ni Waafrika wenzao. Tofauti na *Kinjeketile* ambayo inawasilisha suala la kihistoria hasa katika harakati za ukombozi kutoka katika ukoloni mkongwe, ukoloni chini ya Mjerumani.

Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa tamthiliya hizi zinatofautiana katika kutumia ufundi wa kisanii katika uteuzi na matumizi ya lugha kibunifu katika kuwasilisha dhamira mbalimbali. Ubunifu huu ni tofauti na tamthiliya ya *Kinjeketile* ambaye ametumia lugha ya mazungumzo ya kawaida amabyo hayampi nafasi msomaji kufikiri dhamira ya mwandishi kwa mfano katika uk. 5 anasema ówewe mwanamke Wamatumbi waogaô, ósisi sote tunataka Njerumani aondokeô Lugha iliyotumika katika mifano hiyo ipo wazi na msomaji anaweza kuitafsiri bila shida. Tofauti na Morani ambayo

inamfanya msomaji atafsiri dhamira ya mtunzi katika matumizi ya sitiari, taswira na picha alizotumia kujenga dhamira hizo.

Kwa upande mwingine, tamthiliya hizi zinatofautiana katika matumizi ya vipengele vya lugha. Kwa vile *Kinjeketile* imejengwa kwa kutumia lugha ya kawaida na rahisi, ilibainika kuwa kuna baadhi ya vipengele vya lugha ambavyo havijatumika. Tofauti nyingine ni kwamba, katika *Kinjeketile* kuna matumizi ya methali moja tu tofauti na *Morani* ambaye ametumia methali 7 katika kujadili suala zima la unyonyaji, uhujumu uchumi na harakati za ukombozi na ujenzi wa jamii mpya.

Tofauti nyingine ni suala la kihistoria ambalo tamthiliya hizi zinawasilisha; *Morani* inatumia fasihi simulizi kuwasilisha suala la kihistoria la jamii ya Tanzania huru katika harakati za ujenzi wa jamii mpya yenye usawa na umiliki sawa wa mali. Jamii isiyokuwa na matabaka na kuundoa ukoloni mkongwe. Tofauti na *Kinjeketile* ambayo inatumia lugha rahisi na ya kawaida kuwasilisha suala la harakati za ukombozi kutokana na ukoloni wa Mjerumani. Inahusu jamii inayotawaliwa na wakoloni.

Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa zipo mbinu za kimtindo ambazo zinazitofautisha tamthiliya hizi. ilibainika kuwa tamthiliya ya *Morani* imetumia mbinu za kisanii zaidi katika kuwasilisha suala la kihistoria. Mbinu zilizotumika kama vile; kisitiari, korasi, majigambo, motifu ya safari zinaifanya tamthiliya ya *Morani* ionekane kuwa ni tamthiliya yenye ófumboô ama kitendawili kinachotakiwa msomaji atumie mbinu za uhakiki wa kifasihi katika kukitegua. Mbinu za kimtindo zilizotumika katika tamthiliya hizi zinatofautiana katika kiwango cha utumizi na kumbainisha upekee wa

mtunzi kutokana na athari za kimazingira ya kijiografia na kihistoria. Kwa ujumla tamthiliya ya Morani ni tamthiliya ya Majaribio ambayo imetumia zaidi mbinu za fasihi simulizi ya Kiafrika katika kuwasilisha maudhui yake.

Kwa mfano matumizi ya wimbo, majigambo, wahusika wasio watu kama vile Dongo wahusika wa kufikirika. Utafiti huu unaichukulia tamthiliya ya *Kinjeketile* kama tamthiliya iliyojikita katika utunzi wa Kiaristotle kwa sababu inazungumzia juu ya mhusika aliyeaminiwa na watu na hatimaye kuanguka. Vile vile, ni tamthiliya ambayo imejikita zaidi katika majibizano ya wahusika.

Utafiti huu uligundua kuwa, tamthiliya ya *Kijeketile* na *Morani* zinatofautiana zaidi kuliko kufanana. Kufanana kwa tamthiliya hizi kunatokana na sababu kwamba zote zinawasilisha masuala ya kihistoria japo kwa mbinu tofauti za kisanaa na pia vipindi tofauti vya kihistoria. Hivyo basi, ni vigumu sana kutoa hitimisho kuwa tamthiliya hizi zinafanana.

Utafiti huu uligundua kuwa tamthiliya hizo zinafanana katika matumizi ya sitiari, tashibiha, tashihisi na takriri. Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa tamthiliya hizi zinafanana katika kuwasilisha dhamira mbalimbali kwa kutumia vipengele vya lugha. Dhamira kama vile; unyonyaji na ukandamizaji, hali ngumu ya uchumi, mapinduzi na harakati za ukombozi, rushwa, matabaka, nafasi ya mwanamke, uongozi mbaya na matumizi mabaya ya madaraka. Utafiti huu uligundua kuwa, wasanii wote wawili wanafanana katika dhamira ambazo wameibua katika kazi zao za fasihi hii ni kutokana na ukweli kwamba wasanii wote wanatoka katika jamii zenye historia zinazofanana, itikadi moja, uchumi, siasa, na zinafanana kijamii,

kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Athari za ukoloni kwa jamii zao na kwa wasanii inawafanya watunzi wafanane.

### 5.3 Hitimisho

Utafiti huu umejadili kuwa, vipengele vya lugha ambavyo vimetumika katika tamthiliya zilizochunguzwa katika utafiti huu ambazo ni *Morani* na *Kinjeketile.* Utafiti huu umebaini kuwa tamthiliya ya *Morani* imetumia vipengele vya lugha kama vie tamathali za semi, metahali na semi. Utafiti huu umebaini kuwa, *Morani* imetumia lugha ya kitamathali zaidi katika kuwasilisha maudhui ya kazi yake na hivyo kumfanya msomaji aweze kufikiri zaidi ili kuweza kubaini kile msanii alichokusudia.

Tofauti wakati *Kinjeketile* ambayo imetumia lugha ya kawaida na iliyo wazi zaidi ambayo haimtaki msomaji kufikiri ili kuweza kubaini kile anachokiwasilisha msanii. Imejadiliwa kuwa vipengele vya lugha vilivyotumika katika tamthiliya teule vimelenga kuwasilisha dhamira kuu za tamthiliya hizo kama vile ujenzi wa jamii mpya, harakati za ukombozi na mapinduzi, hali ngumu ya uchumi, nafasi ya mwanamke, unyonyaji na ukandamizaji, rushwa na usariti.

Katika kuzilinganisha na kuzitofautisha tamthiliya za *Morani* na *Kinjeketile,* tamthiliya hizi zinatofautiana katika mbinu za kisanii na ubunifu. Tamthiliya ya *Morani* imetumia mbinu na lugha ya kitamathali katika kuwasilisha ujumbe na maudhui yake wakati tamthiliya ya *Kinjeketile* imetumia lugha ya kawaida, rahisi na ya wazi zaidi katika kuwasilisha maudhui yake. Aidha utafiti huu umebaini kuwa, tamthiliya hizi zinatofutiana katika kuwasilisha suala la kihistoria kwa sababu

wasanii wanawasilisha historia ya jamii ya Tanzania katika vipindi viwili tofauti.*Morani* anawasilisha historia katika kipindi cha baada ya uhuru na hivyo kujadili juu ya historia ya harakati za kupambana na ukoloni mamboleo wakati *Kinjeketile* inajadili kwa uhalisia juu ya harakati za jamii za kusini katika kupambana na ukoloni wa Mjerumani, yaani, na imani ya maji yanayoweza kuibadili risasi kuwa maji.

Kwa upande mwingine ilibainika kuwa tamthiliya hizi kwa vile zimendikwa na wasanii wa jamii moja ambao wameshuhudia na kupata masimulizi ya historia ya jamii yao. Wasanii hawa wanafanana katika kuwasilisha maudhui ya kazi zao ambapo wote kwa pamoja wanajadili juu ya mambo mbalimbali yaliyopo katika jamii kama vile; rushwa, harakati za ukombozi, usaliti, unyonyaji na ukandamizaji, kusoma katika na kubaini kuwa tamthiliya ya Aidha, sura hii imebainisha na kujadili dhima za vipengele vya lugha katika tamthiliya teule.

Kulingana na utafiti huu, tunaweza kuona faida ya utafiti huu kwa taaluma ya fasihi na jamii kwa ujumla. Kwanza kupitia utafiti huu utachochea ari ya kufanyia utafiti kazi mbalmbali za kifasihi hususani tamthiliya ya Kiswahili pia katika tamthiliya zinazozungumzia historia fulani ya nchi kwa kuona namna ambavyo kazi hii ya kiutafiti ilivyofanikiwa. Pili kupitia utafiti huu umeleta faida kubwa kwa wasomi kwani utatajirisha maktaba zetu ikiwemo ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambapo wasomi watasoma na kupata rejea ya mambo mbalimbali ya kimtindo na watafiti wengine wakiutumia utafiti huu kwenye kazi zao tangulizi.

Tatu kupitia utafiti huu umesaidia kukuza lugha kwani vipengele vya lugha vilivyofafanuliwa namna vilivyotumika katika kazi hizo za kifasihi kama vile matumizi ya tamathali za usemi, wale watakao kuwa wanaisoma kazi hii watakuwa wanakuza msamiati na matumizi ya lugha kiusanii. Nne utafiti huu umewafaa sana wanafunzi wa sekondari na wale wa Vyuo Vikuu ambapo itawarahisishia kuvibaini vipengele vya kimtindo na dhima yake katika kuwasilisha suala la kihistoria. Tano utafiti huu umetoa mchango wake kwa jamii kwa kutaka kuonesha umuhimu wa historian a namna gani kazi mbalimbali za kifasihi hubeba historia ya nchi.

## 5.4 Mapendekezo

Kwa kutumia utafiti huu tumeweza kulinganisha tamthiliya za kihistoria, utafiti huu unahitimisha kuwa Tamthiliya ya *Morani* na *Kenjeketile* ni Tamthiliya ambazo zinatofautiana katika uteuzi na utumizi wa vipengele vya lugha na ubunifu wa kisanii, pia ni tamthiliya zinazowasilisha historia za nyakati mbili tofauti. Hivyo basi, utafiti huu unapendekeza kwamba ipo haja ya kufanya utafiti wa kina zaidi kuhusu kazi za tanzu zingine zilizoandikwa kuhusu historia ya jamii ikimaanisha kuwa watafiti wengi wajitokeze kufanya utafiti unaojikita katika kazi za kisanii za kihistoria pia wasanii mbalimbali wajitokeze katika kutunga kazi za kifasihi zenye kubeba historia ya jamii hususani katika tamthiliya ya kiswahili, pia tafiti mbalimbali zifanyike kwani zitakuza lugha na zitasaidia wanafunzi wa Sekondari na Vyuo kutumia kazi hizo za kiutafiti kama rejea zao, pia kuwahamasisha katika kufanya utafiti. Kwa kufanya hivi tutaweza kutoa hitimisho la jinsi wasanii wanavyoweza kutumia ubunifu katika kuwasilisha suala la kihistoria katika tanzu zingine tofauti na tamthiliya.

## MAREJELEO

Alderson, C.G. & Beretta, A. (1992). (Wah.) *Evaluating Second Education: Cambridge Applied Linguistics*, C.U.P.

Bachman, R. & Schutt, R. (2007). *The Practice of Research in Criminology and Criminal Justice* (Toleo la 3). Thousand Oaks, CA: Sage.

Baker, T. (1994). *Doing Social Research*. Singapore: McGraw-Hill.

Bryman, A. (2004). *Social Research Methods* (Toleo la 2). Oxford: Oxford UniversityPress.

Best and Kahn, J. (1993). *Research in Education*. New York: Allyn Bacon Inc.

Borg, W.R and Gall, M.D, (2003). *Educational Research: An Introduction*. Longman London.

Corbetta, P. (2003). *Social Research: Theory, Methods and Techniques*. London: Sage Publications Inc.

Cooper, H. (1989). *Homework.* White Plains, NY: Longman.

Cuddon, J.A. (1998). *Dictionary of Literarry Terms and Literary Theory*, Great Britain: AndreDeutsch.

Daymon, C. and Holloway, I. (2002). *Qualitative Research Methods in Public Relations and Marketing Communications*. London: Routledge.

De Vaus, D. A. (1993). *Surveys in Social Research* (Toleo la 3.). London:UCL Press.

Eagleton, T. (1983). *Literary Theory: An Introduction. Cambridge:* Blackwell.

Halliday, and Hassan, (1976). *Cohesion in English*. London and NY: Longman.

Holloway, L. (1997). *Basic Concepts for Qualitative Research*. Oxford: Blackwell Science.

Hussein. E. (2003). ñHatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga Tamthiliya Kufuatana na Misingi ya Ki-Aristotle.ò Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 111 FASIHI*. TUKI. Dar es Salaam.

Hussein, E. (1969). *Kinjeketile*. Oxford University Press, Nairobi.

Jakobson, R. (1960). óClosing Statement: Linguistics and Poetics.ô In: Thomas A. Sebeok, ed.,*Style In Language*, Cambridge MA: MIT Press, uk. 350-377. Iliyochapishwa katika J.-J. Weber, ed., *The Stylistics Reader*, London: Arnold, 1996, uk. 10-35.

Jilala, H. (2008). The Artistic Uses of Metaphors in Constructing Meanings and Messages in New Generation Songs in Tanzania, Tasnifu ya Umahiri (Isimu) haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kahigi K.K. (1995). Lugha Katika Vitabu Vya Watoto. Katika Kahigi K.K. (mh), Kioo cha lugha: *Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi*. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Juzuu, Na. 1. (uk. 21-36).

Kezilahabi, E. (1976). *Ushairi wa Shaaban Robert*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Kiango, S. D. (1980). *"Tamthiliya ya Kiswahili na Mabadiliko ya Dhamira 1957-1975"* Tasnifu ya Umahiri., Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Kiango, S. D. (1982). ñTamthiliya ya Kiswahili: Dhamira Chapwa na Usuli katika Uchapwaò. *Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi*. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es salaam Juzuu Na, 49/2 (uk:33-56).

Kingôei (1987). ñUsanifu wa Lugha katika Uandishi wa E.Hussein.ò Katika *Mulika Na. 19.* TUKI.

Kingôei, K. na Catherine Kisovi (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*, Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kombo, D.K. and Tromp, D. L.A, (2006). *Proposal and Thesis Writing: Intoduction*, Kenya, Paulines Publications Africa.

Kothari, C. K (1990). *Research Methods: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C.R. (1993). *Research Methodology: Methods and Techniques (Toleo la 2)*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kvale, S.(1996). *Interviews An Introduction to Qualitative Research Interviewing*. London: Sage Publications.

Lakoff, G. and Johnson, M. (1980). *Metaphor We Live By*. Chicago: University of Chicago Press.

Lakoff, G. and Turner, M. (1989). *More Than Cool Reasons. A Field Guide to Poetic Metaphor*. Chicago: University of Chicago Press.

Lakoff, G. & Johnson, M. (1988). *Metaphors we Live By (Toleo la 2.)*: Chicago: Chicago University Press.

Lanham, R A. (1991). *A Handlist of Rhetorical Terms* London: University of California Press.

Leech, G.N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. New York: Longman Group Inc. Limited.

Lee, R.M. (1993). *Doing Research on Sensitive Topics*. Londo:Sage.

Malangwa, P.S. (2010). ñHandling Technical Translations: The Case of Translatins of ComputerPrograms from English into Kiswahili.ò Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa),ChuoKikuu cha Dar es Salaam.

Mauya, A. B. (2006). *Semi Maana na Matumizi*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mayoka, J. M. (1984). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*, Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mbogo, E. (1993). ñMatumizi ya Dhana na sanaa katika Sanaa za Maonyesho za Jadi katika Tamthiliya ya Leo.ò Katika Mulokozi na Mungôongôo (Wah): 181-206.

Mbogo, E. (2007) Morani Macmillan Aidan Ltd Dar es Salaam.

Mlama, P. (1983). Traditional Theatre as A Pedagogical Institution: The Kaguru Theatre as Case Study. Ph.D. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

Mlama. P.O. (2003). ñUtunzi wa Tamthiliya Katika Mazingira ya Tanzania.ò Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 111 FASIHI*. TUKI. Dar es Salaam.

Hussein I.N. (1970). *Kenjeketile* . Oxford University Press, Nairobi.

Msanjila, Y.P., Kihore, Y.M. na Massamba, D.P.B. (2009). *Isimujamii: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. EAEP, Nairobi.

Mugenda, O.M. na Mugenda, A.G. (2003). *Research Methods*: *Qualitative and Quantitative Approaches*. Nairobi: Acts Press Kenya.

Mulokozi, M. and Kahigi, K.K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: TPH.

Mulokozi, M. M. (1986). ñThe Nanga Epocs of the Bahaya: A Case Study in African Epic Characteristicsò, Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

(1997). ñKorasi na Uhusiano Wake na Sanaa za Maonyesho: Uchambuzi wa Kidaikronia.ò Katika *Kioo cha Lugha*. Juzuu Na. 2. Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M.. (2012). *Korasi katika Fasihi: Nadharia Mpya ya Uhakiki*. Taaluma ya Taasisi za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Njogu, K. na Chimerah, R.M. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi: Jomokenyatta Foundation.Tanzania.

Mutembei, K.A. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkwera, F. V. (1979). *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo*, Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Padgett, D. (2002). *Qualitative Methods in Social Work Research: Challenges and Rewards.* London: Sage Publications Inc.

Patton, M. (2002). *Qualitative Research and Evaluation Method* (Toleo la 3). London: Sage Publications.

Peek, P. M. na K. Yankah (wah.) (2004). *African Folklore: An Encyclopedia*, London na New York: Routledge Taylor and Francis Group.

Polit, D. F., Beck, C. T. and Hungler, B. P. (2001). *Essentials of Nursing Research: Methods,Appraisal and Utilization*, 5th edn. Lippincott, Philadelphia.

Powell, R., Conway, C., & Ross, Lynda. (2004). Effects of student predisposing characteristics on student success, *Journal of Distance Education,* Vol. 5, No. 1, pp. 20-37.

Powell, R. R. & Lynn Silipigni Connaway. (2004). *Basic Research Methods for Librarian*(Toleo la 5.). London: Sage Publications Inc.

Punch, K. F. (2005). *Introduction to Social Research: Qualitative and Quantitative Approaches*(Toleo la 2.). London: Sage Publications Inc.

Ramadhani, D. (2005). *The Uses of Metaphors in Mbogo's Ngoma ya Ng'wanamalundi and Hussein's Morani. A Stylistic Comparison.* Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa) University of Dar es Salaam.

Schutt, R. K. (2006). *Investigating the social world: The process and practice of research*. London: Sage Publications.

Semzaba, E. (2003). *Tamthiliya ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.Tanzania.

Silver, H.(1995). óReconceptualizing Social Disadvantge: Three Paradigms of Social Exclusion.ô In *Social Exclusion: Rhetoric, Reality, Responses*. imehaririwa na Gerry Rodgers, Charles Gore, and Jose Figueiredo. Geneva: International Institute for Labour Studies.

Silva, M. (1995). *Ethical Guidelines in the Conduct, Dissemination, and Implementation of Nursing Research.* Washington DC: American Nurses Publishing.

Silverman, D. (2005). *Doing Qualitative Research: A Practical Handbook* (Toleo la 2.). London: Sage Publication Inc.

Speziale, H.J. S. & Carpenter, D.R. (2007). *Qualitative Research in Nursing:*Advancing the humanistic imperative (Toleo la 4). Philadelphia: Lippincott.

Speziale, H.S. and Dona R. Carpenter.( 2006). *Qualitative research in Nursing: dvancing theHumanistic Imperative*. Philadelphia: Lippincott Williams and Wilkins.

TUKI. (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. (Toleo la 2). Nairobi: Oxford University PressTurner, G.W. (1973) *Stylistics*. London: Penguin.

Wafula, R.M. (1999). *Uhakiki wa Tamthiliya*: *Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila K.W (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila K.W (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Focus Publication Ltd. Nairobi Kenya.

Wamitila K.W (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publisher.

Wamitila K.W (2010). Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi. Vide _muwa,Nairobi, Kenya.

Wa Thiongõo, Ngugi. (1995). *Decolonising the mind: The language of literature in Afrika.* London: Curey Publishers.

Weiss, R. S. (1994). *Learning from strangers: The art and method of qualitative interviewing.*New York: Free Press.

# VIAMBATISHO

## Kiambatishi 1:Mwongozo wa Maswali ya Usaili kwa Ajili ya Wanafunzi wa Fasihi, Walimu wa Fasihi na Watu wa Karibu wa Watunzi

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu **Dhima ya Mtindo katika Tamthiliya za Kihistoria: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya *Morani* na *Kinjekitile*.**Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhima ya vipengele vya kimtindo katika tamthiliya za kihistoria kwa kulinganisha tamthiliya za *Morani* na *Kinjeketile* ili kubaini vipengele vinavyowafananisha na kuwatofautisha wasanii wa vitabu hivyo katika kuliwasilisha suala la kihistoria. Nitashukuru sana kama utajibu maswali haya kwa makini, uwazi, usahihi, kwa kujitolea na ushirikiano wa hali ya juu. Kumbuka taarifa zote zitakazotolewa zitahifadhiwa kama siri baina ya mtafiti na mhojiwa na pia zitatumika kwa ajili ya utafiti huu tu na si vinginevyo.

1. Je, ni vipengele vipi vya lugha vinavyojitokeza katika *Morani* na *Kinjeketile*?
2. Je, katika vipengele hivyo ni vipengele vipi vimebeba maudhui ya kihistoria?
3. Je, ni vipengele vipi vinavyowafananisha ama kuwatofautiha na au kuwahusianisha wasanii wa tamthiliya hizi?
4. Unafikiri watunzi wa tamthilia ya *Morani* na *Kinjeketile* walishughulikiaje suala la Kihistoria kwa kutumia vipengele vya lugha? Toa mifano ya vipengele vya lugha vinavyosawiri suala la historia ya jamii
5. Unafikiri ni kwa nini watunzi hawa wanafanana?

6. Je, unafikiri ni kwa nini wanafanana? Toa mifano kutoka katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile*
7. Je, ni kweli kwamba Emanuel Mbogo wa *Morani* na Ebrahimu Hussein wa *Kinjeketile* wanatofautiana katika utumizi na uteuzi wa vipengele vya lugha?
8. Je, unaweza kueleza sababu kwa nini watunzi hawa wanatofautiana kimaudhui na kifani?

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**Kiambatishi 2:Mwongozo wa Maswali ya Usaili Kwa Ajili ya Watunzi wa Tamthilia ya Morani na *Kenjeketile***

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu **Dhima ya Mtindo katika Tamthiliya za Kihistoria: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya *Morani* na *Kinjekitile***. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhima ya vipengele vya kimtindo katika tamthiliya za kihistoria kwa kulinganisha tamthiliya Morani na Kinjeketile ili kubaini vipengele vinavyowafananisha na kuwatofautisha wasanii wa vitabu hivyo katika kuliwasilisha suala la kihistoria. Nitashukuru sana kama utajibu maswali haya kwa makini, uwazi, usahihi, kwa kujitolea na ushirikiano wa hali ya juu. Kumbuka taarifa zote zitakazotolewa zitahifadhiwa kama siri baina ya mtafiti na mhojiwa na pia zitatumika kwa ajili ya utafiti huu tu na si vinginevyo

1. Ni kwa nini uliamua kuita jina hili la tamthilia yako?
2. Je, ni msukumo gani uliokusukuma kuandika tamthiliya yako kwa namna ulivyoiandika?
3. Je, kuna mtunzi yeyote aliyekuathiri ama kwa kuiga utunzi wake? Tafadhali naomba umtaje jina lake.
4. Unafikiri tamthiliya yako imeiga ama kuathiriwa na tamthiliya uliyoitaja hapo juu katika uteuzi na utumizi wa vipengele vya lugha?
5. Unadhani mbinu za kimtindo ulizozitumia zimeleta ufanisi wa ujumbe uliotaka kuutoa?

***ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO***

**Kiambatishi 3:Dodoso kwa Walimu wa Fasihi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu **Dhima ya Mtindo katika Tamthiliya za Kihistoria: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya *Morani* na *Kinjekitile*.**Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhima ya vipengele vya kimtindo katika tamthiliya za kihistoria kwa kulinganisha tamthiliya *Morani* na *Kinjeketile* ili kubaini vipengele vinavyowafananisha na kuwatofautisha wasanii wa vitabu hivyo katika kuliwasilisha suala la kihistoria. Nitashukuru sana kama utajibu maswali haya kwa makini, uwazi, usahihi, kwa kujitolea na ushirikiano wa hali ya juu. Kumbuka taarifa zote zitakazotolewa zitahifadhiwa kama siri baina ya mtafiti na mhojiwa na pia zitatumika kwa ajili ya utafiti huu tu na si vinginevyo:

**Maelezo Binafsi**

Jina la mhojiwaé é é é é é é é é é é é é .é é é é é ..é é é é é é é é é

Umrié é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é é é .é é é é é é é é é ..

Jinsié é é é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é é é é é é é é é é

Tareheé é é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é é é é é é é é é é

1. Vipengele vya lugha katika tamthilia za *Morani* na *Kinjeketile* vina dhima gani katika kazi hizi za fasihi?

    (i) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é é é é é

    (ii) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é é é é é .

    (iii) é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é é é é é é é é é é é .

    (iv) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é ..

    (v) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é é é é é .

2. Nini uhusiano wa kipindi cha kihistoria cha kutungwa kwa kila tamthiliya?

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

3. Na utumizi wa vipengele vya lugha? é é é é é é é é é é é é é é é é ..

4. Unafikiri ni nini lengo la mwandishi katika kutumia mbinu mbalimbali za kimtindo katika utunzi wa tamthiliya zao?

(i) é é é é é é é é é é é .é é é ..é é é é é é é é é é é é é é é .

(ii) é é é é é é é é é é .é é é é é é é .é é é é é é é é é é é é ..

(iii) é é é é é é é é é é é é é é é ..é é é é é é é é é é é é é é ..

(iv) é é é é é é é é é é é é ..é é é é é é é é é é é é é é é é é ..

(v) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é

***ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO***

**Kiambatishi 4:Dodoso kwa Wanafunzi Wakozi ya Fasihiwa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu **Dhima ya Mtindo katika Tamthiliya za Kihistoria: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya *Morani* na *Kinjekitile***. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhima ya vipengele vya kimtindo katika tamthiliya za kihistoria kwa kulinganisha tamthiliya *Morani* na *Kinjeketile* ili kubaini vipengele vinavyowafananisha na kuwatofautisha wasanii wa vitabu hivyo katika kuliwasilisha suala la kihistoria. Nitashukuru sana kama utajibu maswali haya kwa makini, uwazi, usahihi, kwa kujitolea na ushirikiano wa hali ya juu. Kumbuka taarifa zote zitakazotolewa zitahifadhiwa kama siri baina ya mtafiti na mhojiwa na pia zitatumika kwa ajili ya utafiti huu tu na si vinginevyo;

**Maelezo Binafsi**

Jina la Mhojiwaé é é é é é é é é é é é é é é é é é é é ..é é é é é é é

Umrié é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é

Jinsié é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é .

1. Taja vipengele vya lugha vinavyojitokeza katika tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile.*

   (i) é é é é é é é é .é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é .

   (ii) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é é é é .

   (iii) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é é é é é é é .

(iv) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é é é é é é é .

(v) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é é é é é é é .

2. Vipengele hivyo vina dhima gani ya kifasihi?

(i) é é é é é é é é .é é é é é é é é é é é .é é é é é é é é é é

(ii) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é .é .é é é é é é

(iii) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é .é é .é é é é é é é é é é

(iv) é é é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é .é é é é é é é é é é

(v) é é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é é .é é é é é é é é é é

3. Je ni vipengele vipi vya lugha vinavyozitofautisha tamthiliya ya *Morani* na *Kinjeketile?*

(i) é é é é é é é é .é é é é é é é é é é é .é é é é é é é é é é

(ii) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é .é .é é é é é

(iii) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é .é é .é é é é é é é é é

(iv) é é é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é .é é é é é é é é é

(v) é é é é é é é é é é é é é é é é .é é é é é .é é é é é é é é é

4. Je ni vipengele gani vya lugha vinavyozifananisha tamthiliya hizo?

5. Je unafikiri ni sababu zipi zinazowafanya wafanane ama kutofautiana?

***ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO***